# *Nini Kinachovutia Kule Mlimani?*

Amini tu, amini tu,
Yote yatendeka, amini tu.

Na tuinamishe vichwa vyetu sasa:

Baba Mungu, hilo ndilo ombi letu aminifu usiku wa leo, tunapoona yote unayowatendea watu siku hizi. Ndipo tunakuomba, Bwana, na tuamini tu, tuamini tu ya kwamba Hiyo ni Kweli, Neno lililoandikwa likidhihirishwa kwetu. Tujalie mambo haya, Baba.

2 Sasa, usiku wa leo tunataka kukushukuru kwa ajili ya—ya Nuru uliyoangazia Maandiko kwa ajili yetu asubuhi ya leo. Na tunaomba usiku wa leo, Bwana, kwenye mstari wa maombi, ya kwamba utathibitisha Neno Lako Kweli.

3 Tunayaombea makanisa yote na makusanyiko ambayo yamekusanyika kuzunguka vile—vile—vile vipaza sauti vidogo nchini kote, kutoka kwenye taifa, kote kote hata kwenye Pwani ya Magharibi, kule juu kwenye milima ya Arizona, chini kwenye mabonde ya Texas, mbali sana hata Pwani ya Mashariki, nchini kote, Bwana, ambako wao wamekutanika. Tuko umbali wa masaa mengi, bali, Bwana, sisi tuko pamoja usiku wa leo kama jamii moja, waamini, tukingojea kuja kwa Masihi. Nasi tunaomba, Baba wa Mbinguni, ya kwamba Wewe utamtuma hivi karibuni kwa ajili ya Kanisa Lako. Kwani tunaomba hayo katika Jina Lake. Amina. (mwaweza kuketi)

4 Salamu za Kikristo kwa nyote mlio hapa usiku huu. Nasikitika ya kwamba tungali tumesongamana na kufinyana hata ni shida kwetu kupumua. Hata vyombo vya kubaridisha, hata vikifanya kazi vipi, havifai sana, watu wengi sana. Kama ingalikuwa tu kanisa la kawaida lililojaa watu, vyombo hivyo vingewagandisha. Bali sasa kila mmoja ana pepeo, akijipepea, na vyombo vya kubaridisha hewa vikivumisha kwa nguvu iwezekanavyo.

5 Tunatuma salamu kutoka Pwani ya Mashariki hata Pwani ya Magharibi, kwa marafiki wetu wote katika Kristo wanaosikiliza. Tunatuma salamu zetu kule San Jose, Ndugu Borders, kile kikundi kule juu. Tunazituma kule milimani katika Prescott, Arizona, kwa Ndugu Leo Mercier pamoja na kundi lake lililo kule juu linalongojea kule Kuja kwa Bwana. Tunatuma salamu kwa wale walioko Tucson waliokusanyika usiku wa leo, wakingojea kule Kuja kwa Bwana. Chini katika Houston, Texas, kwa wale wanaongojea Kuja kwa Bwana. Kule juu Chicago,

kwa wale wanaongojea Kuja kwa Bwana. Kule juu kwenye Pwani ya Mashariki, New York na Connecticut, na vile vikundi vikubwa kule vinavyongojea Kuja kwa Bwana. Hatuna nafasi hapa wanakoweza kuketi, kwa hivyo inatulazimu tu kuwatumia Neno kwa nji—njia ya simu. Tunatuma salamu zetu kwa Ndugu Junior Jackson usiku wa leo, na kundi lake kule Clarksville. Ndugu Ruddell kule 62, na kundi lake, wanaongojea kuja kwa Bwana. Nasi tumekusanyika hapa usiku wa leo katika kanisa la nyumbani, yale Maskani, tukingojea kuja kwa Bwana.

6 Na sasa, wengi wenu huenda ikawa hawakuweko kwenye ibada asubuhi ya leo. Lakini natumaini ya kwamba kila mmoja ambaye hakuwako atapata hiyo kanda, kwa maana naamini huo ulikuwa ujumbe moja kwa moja sana kwa kanisa tangu ule—ule ujumbe wa *Mabwana Ni Wakati Gani*? Nilihisi upako wa Roho, nikajisikia nikiongozwa kusema yale niliyosema. Ulikuwa mrefu, ingawaje nilijisikia nikiongozwa kufanya hivyo. Nami nafikiri Bwana, kwa Neno Lake, alionyesha ni majira gani tunayoishi. Natuhakikishe ya kwamba tunaelewa mambo haya ya ajabu yanayotendeka. Mwajua, Biblia ilisema, “Wao walio na hekima ndio watakaoelewa.”

7 Bali mataifa pamoja na watu watazidi kuwa wanyonge na werevu. Hebu fikiria, Mmarekani wastani sasa hufikia umri wa kati yapata miaka ishirini, mnyonge bali mwerevu. Wao hawakuwa na eropleni siku hizo, na—na makombora ya atomiki, bali waliishi miaka mingi zaidi. Sisi tunazidi kuwa wanyonge na werevu, na werevu wetu ndio utakaotuangamiza. Tutajiangamiza wenyewe. Mungu hatatuangamiza, werevu wetu utatuangamiza. Imekuwa hivyo daima, na itakuwa hivyo tena.

8 Basi Bwana akitujalia, Jumapili ijayo asubuhi, sijui nitahubiri nini, bali natumaini ya kwamba Bwana, iwapo atatuuruhusu kuishi na kusitendeke cho chote, na iwe ni mapenzi Yake, tunatarajia kuhubiri ujumbe mwingine Jumapili ijayo asubuhi, tuwe na maombi kwa ajili ya walio wagonjwa Jumapili usiku. Ndipo itanilazimu kurudi Arizona, kuwarudisha jamaa yangu kule ili watoto wapate kujiandikisha shuleni. Ndipo nanyi mta... Tutawaarifu, tuwezavyo, juu ya mikutano inapotayarishwa, ama nyakati ambazo tuna... mahali ambapo tunatarajia kuwa. Kwa hiyo Mungu awabarikini nyote.

9 Sasa usiku wa leo, tunapojua ya kwamba ni... Kwanza nimechelewa kwa muda wa dakika kumi na tano, saa mbili kasorobo hapa Jeffersonville, na hiyo ni kama saa tatu kasorobo kule—kule Pwani ya Mashariki; na ndipo yapata saa kumi na moja kwenye Pwani ya Magharibi. Kwa hivyo tuko karibu machweo ya jua hapa. Nami nataka kunena nanyi kwa ibada fupi tu, kujaribu kupata upako wa Roho na ndipo niite mstari wa maombi.

10 Nami nataka makutano haya hapa na makutano waliokutanika mahali penginepo, wampate mtu fulani, ndugu ye yote mwenye upako wa Roho, na tunapoanza kuombea wagonjwa, aende akawawekelee mikono wale walio kwenye makutano yenu. Na, kumbuka, Mungu yuko mahali pote, ameenea kila mahali. Kwa hivyo, kule chini Texas, kule juu California, juu kule Arizona, po pote mlipo, wawekeleeni wagonjwa mikono tutakapoanza kuwaombea wagonjwa. Nami nina hakika Mungu atayasikia na kujibu maombi.

11 Jambo ng'eni, Jumapili iliyopita usiku, nao upako ulikuwa unaendelea, na Roho Mtakatifu . . . Ilikuwa jambo la ajabu. Sikuwa nimekuwa na m—mstari wa utambuzi kwa miezi na miezi, tangu nilipokuwa hapa wakati uliopita. Na ndipo kwenda pale kwa ahadi . . . Haujui kama Yeye ataitimiza. Huwezi kusema ataitimiza. lnakupasa tu kwenda pale na kungojea. Yeye ni mwenyezi, hutenda anayotaka. Lakini kusimama pale na kungoja, kuona atakayotenda, ndipo unasikia ikikujilia hivyo.

12 Na mwisho wa u—ule mkutano, bila kujua ilikuwa nani, bali palikuwapo m—mtu mahali fulani mstarini aliyekuwa mrefu, mwenye upara, naye alikuwa mgonjwa sana.

13 Na ndipo mwishowe pakatokea mtu fulani hapa jukwaani, naye ameinamisha kichwa chake, naye alionekana mwenye kuugua, ameshika tumbo lake. Nami nikadhani huenda huyo akawa yule mtu wa kwanza ama mtu wa pili, ama po pote ilipokuwepo ambaye nilimwombea, maana alikuwa na upara na ameinamisha kichwa chake; mtu mkubwa, aliyeinama. Bali nikatazama huku na kule na kumwona yule mwungwana ameketi kule, bali alikuwa mwenye furaha. Nikawaza, "Ni wapi?" Singeweza kuamua ilikuwa wapi. Ningelihisi na kumwona yule mtu mbele zangu. Nikaihisi ikivuta upande huu, nayo ilikuwa ikitoka nyuma. Nikamtazama Ndugu Neville na hawa wawili walioketi hapa, haikuwa wao. Nikasema, "Mtu huyo yuko upande wa ndani wa kile chumba cha kubatizia nyuma kule." Na mnajua ilikuwa nani? Ndugu Shepherd. Sababu ya kutokumtambua, alikuwa ameketi nyuma kule huku kichwa chake kimeinamishwa, akiomba.

14 Yeye alifikiri atakufa, alifikiri hayo kwa majuma kadha yaliyopita. Mke wake alimwambia anunue jozi mpya ya viatu, naye akasema, "Sitazihitaji, sitakuwa hapa muda huo wote."

15 Naye alikutana nami hivi majuzi kwenye . . . kule uwajani kwa Ndugu Wood akipaza sauti na kumsifu Mungu. Kasema, "Ninakula nyama ya nguruwe, mayai, nyanya, cho chote ninachotaka."

16 Na kwa unyenyekevu akatoa kiti chake, na kurudi kule nyuma kabisa, huku akiomba. Unaona, hauhitaji kadi ya maombi, unahitaji tu imani. Unaona? Naam, sijui kama uliponywa ama la, mimi nilisema tu, "M—mtu, anaomba, ana

kasoro." Nafikiri nilitaja ilikuwa nini, "Kuumwa na tumbo, na anaombea nyuma hapa. Bwana Yesu anakuponya." Naam, hiyo tu ndiyo ningemwambia. Mvuto ulikuwa ya kwamba alikuwa yu anaomba. Niliweza kuona hilo, bali yanayotendeka sijui. Unaona?

17 Bali unapoiona ikirudi, kila mmoja anatambua, Inaposema, "BWANA ASEMA HIVI," waona, huyo si mimi ninayenena tena, huyo ni Yeye.

18 Lakini mimi daima husema, "Yesu Kristo amekuponya," hiyo ni Kweli kabisa. "Alijeruhiwa kwa makosa yetu, kwa kupigwa Kwake sisi tumepona." Unaona? Unaona?

19 Bali Inapokuja, "BWANA ASEMA HIVI," na kukwambia ya kutenda na yatakayotendeka, tazama hilo, itakuwa hivyo.

20 Bali ninaposema, "Yesu Kristo anakuponya na kukufanya mzima," amini hilo kwa maana Yeye tayari amesema hayo. Mimi narudia tu yale aliyosema.

21 Na ono ni kurudia tu yale Yeye aliyoonyesha. Mnaelewa?

22 Sasa na tuharakishe tukaingie katika Neno moja kwa moja, kwa sababu najua ya kwamba wengi wenu mlio hapa, mtasafiri maili nyingi usiku wa leo. Naomba ya kwamba Mungu atawabariki na kuwasaidia na kuwalinda barabarani. Na sasa ningetaka kufungua usiku wa leo Mathayo Mt. sura ya 21, na aya 1 hata 11, katika Mathayo Mt. Na, sasa, kama hauna Biblia yako, ama unataka kuandika Maandiko haya, vyema.

23 Na sasa ninyi ambao hamkusikia ule ujumbe asubuhi ya leo, na mna chombo cha kunasia sauti, sisi hatutaki kamwe kuuza kanda. Sisi hatupendelei kuuza cho chote. Wakati mwingine katika mikutano mikubwa watatangaza wana baadhi ya vitabu huko nyuma, hatupati faida yo yote kwavyo, Ndugu Vayle ndiye mwandishi wake. Zile kanda, mtu ambaye hushughulikia kazi ya kanda pale atawaambieni, hatupati pesa kwa kanda. Hatufikirii ya "kanda," ni ule Ujumbe. Na mtu anapofikiria akilini mwake kwamba ni fedha, hatatengeneza kanda tena. Hilo ni sawa. Niliulizia kuhusu hilo, nafikiri kanda zetu zinauzwa kama chini ya dola tano, au kitu kama hicho. Wasema nini? Tatu na nne, kwa hizo kanda kubwa na ndefu.

24 Na muhudumu fulani, niliuliza habari za kanda zake, nazo zilikuwa dola tisa, za dakika ishirini ama thelathini, kwa ujumbe mmoja.

25 Kwa hivyo naona ya kwamba Ndugu yetu Sothmann kule nyuma hatajiriki, ye yote wao, kwa hizi kanda ambazo wana—wanasambaza. Unaona, wanapata tu za kutosha kuendeleza kazi. Siwezi nikawauliza kuzitengeneza bure, kwa maana inawalazimu kununua kanda na vinginevyo. Na hiyo mitambo ni ghali sana, kwanza inagharimu kama dola elfu kumi kuitayarisha kutengeneza kanda hizo.

26 Basi, naelewa kwamba hivi karibuni mimi . . . Wao hawajalitangaza bado, kuna kusikizwa kwa kanda tena. Mara kwa mara sisi . . . wadhamini, mimi sihusiki nayo kamwe. Hata si . . . sijapata kuwa katika wo wote wa mikutano hiyo. Siko upande huu wala ule. Wao hutuma maombi yao, wadhamini huamua ni nani atakayefuata kwa kutengeneza hizi kanda, nao wanamtumia barua. Hayo tu ndiyo ninayojua juu yake. Wao hushughulikia hayo, kwa maana siwezi angaa kuwaweka watoto wakfu sembuse kushughulikia kanda, kwa hivyo . . . au kubatiza.

27 Kwa hivyo moyo wangu wote umo kwenye Ujumbe huu. Huo ndio ule Mvuto wa Tatu, na ndio unaonipasa kuwa mwaminifu na mnyenyekevu kwake.

28 Mathayo 21:1 hata 11. Nilisema hayo tupate kuwa mkitazama . . . ama kufungua Maandiko:

> *Hata walipo—hata walipokaribia Yerusalemu, na kufikia Bethfage, katika mlima wa Mizeituni, ndipo Yesu alipotuma wanafunzi* Wake *wawili,*
>
> *Akawaambia, Enendeni mpaka kijiji kile kinachowakabili, na mara mtaona punda amefungwa, na mwana-punda pamoja naye; wafungueni mniletee.*
>
> *Na kama mtu akiwaambia neno, semeni, Bwana ana haja nao; na mara hiyo atawapeleka.*
>
> *Haya yote yamekuwa, ili litimie neno lililonemwa na nabii, akisema,*
>
> *Mwambieni binti wa Sayuni, Tazama, Mfalme wako amekufa kwako, mpole . . . naye amepanda punda, na mwana-punda, mtoto wa punda.*
>
> *Wale wanafunzi wakaenda zao, wakafanya kama Yesu alivyowaamuru,*
>
> *Wakamleta yu—yule punda na mwana-punda, wakaweka nguo zao juu yao, naye akaketi juu yake.*
>
> *Watu wengi katika ule mkutano wakatandaza nguo zao njiani, na wengine wakakata matawi ya mti, wakayatandaza njiani.*
>
> *Na* makutano *waliotangulia, na wale waliofuata, wakapaza sauti, wakisema, Hosana, Mwana wa Daudi; ndiye mbarikiwa yeye ajaye kwa jina la Bwana; Hosana juu mbinguni.*
>
> *Hata alipoingia Yerusalemu, mji wote ukataharuki, watu wakisema, Ni nani huyu?*
>
> *Makutano wakasema, Huyu ni yule nabii, Yesu wa Nazareti ya Galilaya.*

29 Basi, kama ningechukua somo katika hayo kwa muda wa kama dakika thelathini, kabla mstari wa maombi haujaanza,

ningetaka kuchukua hili kama somo: *Nini Kinachovutia Kule Mlimani?*

30 Naam, ilikuwa siku ya kuchosha na yenye mashaka, na ilikuwa siku isiyo ya kawaida. Tunamwona Yesu hapa akija mpaka Yerusalemu, akiwa tayari kuhudhuria pasaka. Na pasaka ni ambapo mwana-kondoo wa pasaka alivawa, nayo damu ilipakwa kwenye kiti cha rehema kwa ajili ya—ya upatanisho wa—wa watu. Naye alikuwa amefika kutoka Bethfage na alikuwa amefikia kilele cha Mlima wa Mizeituni, ambao unaelekea kilima kingine kidogo ambapo Yerusalemu ilijengwa. Naye alipokuwa akitazama, alijua ya kwamba huku kulikuwa kuzuru Kwake kwa mwisho.

31 Huu ulikuwa wakati ambao angetolewa mikononi mwa wenye dhambi nao wangemuua. Angekufa kifo cha kutisha sana ambacho mwanadamu ye yote amewahi kufa, na kuzikwa. Angesalitiwa na walio Wake, baadhi yao wakisimama papo hapo pamoja naye. Naye, akiwa Mungu, alijua yaliyokuwa mioyoni mwao na alijua tangu mwanzo mtu ambaye angemsaliti. Na alijua ya kwamba mtu huyo alikuwa pamoja Naye ambaye aliketi karibu Naye na kumhesabia fedha Zake, na kadhalika, alijua mtu huyo angemsaliti. Naye alijua ya kwamba msalaba mkatili wa Kirumi ulimngojea kule. Alijua ya kwamba maji mwilini Mwake na Damu ya mwili Wake vingetengana, na ya kwamba Damu ingetiririka kutoka paji la uso wake katika matone makubwa kama jasho. Alijua yote hayo yaliyokuwa mbele Zake. Naye anasimama mlimani, akiutazama Yerusalemu.

32 Watu wa siku hizo, . . . walivyojiita siku hizo "tabaka bora ya watu wa kidini," walimchukia. Makanisa ya siku hizo yalimchukia na kumshutumu hadharani, na kuwashutumu hadharani wote waliomsikiza. Na kama waliondoka na kwenda kuhudhuria mikutano Yake, walifukuzwa mara moja kutoka ushirika wa kanisa. Si ajabu Maandiko yalisema, "Alikuja Kwake, nao walio Wake hawakumpokea." Wale waliopaswa kumpenda, wale waliopaswa kumsaidia, walikuwa adui Zake wa—wabaya sana.

33 Naye akatengeneza kundi Lake ndogo kutoka baadhi ya watu maskini, wavuvi, watoza ushuru, wasio na elimu. Biblia ilisema ya kwamba baadhi yao walikuwa hata "wasio na elimu, wasio na maarifa." Wengine wao hata hawangeandika majina yao. Yeye hakuenda kamwe kanisani kuchagua watu Wake.

34 Naye hakukubaliana kamwe na ye yote wa viongozi wa makanisa. Isitoshe, Yeye alifuata nyayo za nabii hasa, alilaumu cho chote walichofanya, kama wale wengine mbele Yake walivyokuwa wamefanya; kwa sababu wao walikuwa sehemu ya Neno, Naye alikuwa Neno katika ukamilifu Wake.

35 Bali katikati ya hayo yote, kupitia kila wakati na kila nabii ambaye alikuwako ama ambaye angekuwako, kutakuweko kiasi fulani cha watu ambao wamechaguliwa tangu asili kusikia Ujumbe huo, nao wataufuata. Hao hawajali umati wa watu. Hawajali lawama za wasioamini. Wao—wao hawabishani nao. Wana wajibu mmoja, huo ni kuamini na kupata kila sehemu Yake wawezayo, waiingize ndani kama Mariamu aliyeketi miguuni pa Yesu.

36 Naye Maritha alikuwa akimtengenezea chakula Chake cha njioni, naye Yesu akamwambia, "Lakini Maritha, unashughulikia mambo ya maisha, bali Mariamu ametafuta mambo bora zaidi," mwaona, mambo ya Uzima wa Milele.

37 Sasa, tunaona ya kwamba wengi wa watu waliokuwa wameelewa . . . Wao hawakuwa na vitabu kama tulivyo navyo siku hizi, hawakuwa na televisheni ama simu, ama cho chote kile siku hizo, bali kulikuwa na fununu ya kwamba Yeye angehudhuria pasaka. Kwa maana wengi wa watu wale, wakiwa watu wa kiroho, walijua ya kwamba Yeye alikuwa yule Mwana-Kondoo wa Pasaka, kwa maana tayari alikuwa amewaambia mambo ambayo yangetendeka.

38 Na ndipo, bila shaka, wao wakijua ya kwamba Yeye angekuwako, na kumpenda walikompenda, walikuwa wakimngojea. Kulikuwa umati ambao labda ulikuwa ukisukumana, wakibuburushana toka lango hadi lingine, wakiwa macho sana, kwa maana walijua angefika wakati wo wote. Walikuwa macho.

39 Wengine walikuwa wakishangaa watu hawa wana nini kukimbia kutoka lango moja kufikia lingine. "Wanavutiwa na nini?"

40 Nao wangetazama upande *huu* na kutazama *ule,* wakitafuta. Ilionekana kama walikuwa wakitafuta kitu fulani, wenye kutazamia jambo litakalotokea.

41 Jamani, jinsi ningetaka kubadilisha somo langu kwa dakika chache na kusema hivi, ya kwamba hicho ndicho kisa cha siku hizi. Watu ambao wanatazamia kuja Kwake wana hamu sana na matarajio makuu. Tunaweza kuuhisi, ule msongo. Wao wanatafuta, wakiangalia kila tendo na kila ishara, wakizilinganisha na Maandiko.

42 Nao walipoona yale mambo yote yaliyokuwa yamebashiriwa juu Yake, hata mwisho, walijua ya kwamba mwisho umekaribia. Walitaka kuwa huko, kwa hivyo wakawa macho. Sehemu ya umati ule ilikuwa upande Wake, katika uchache. Wengine wao walimpinga, karibu wote, tisini kwa mia walikuwa dhidi Yake.

43 Na hivyo ni kama ilivyo siku hizi kwenye makundi ya kidini, inapofikia Neno na Kristo kweli kweli, kuna yapata asilimia moja ambao wangeamini. Ile sehemu nyingine hawagelijali kamwe, hata ifanywe nini, wao wangelifanyia mzaha ama

kulikashifu. Vile vile tu. Wakati, mambo hayabadiliki sana, historia hujirudia yenyewe pande zote.

44 Vema, tunaona ya kwamba hiyo ilileta wasiwasi. Ilipaswa kufanya hivyo, haina budi kufanya hivyo. Walikuwa wamengoja, walikuwa wakishangaa angefanya nini alipofika huko. Walitaka kuwa huko wakapate cho chote angetenda. Walitaka hilo. Walitaka kuiona. Wao walimwamini. Wengine tayari walikuwa wamesikia ya kwamba Yeye yuaja nao wakaenda kule kumfanyia mzaha. Kwa hivyo baada ya huko kutazamia kote kwenye wasiwasi, siku isiyo ya kawaida sana, wakati usio wa kawaida sana, huku makanisa yamelala, watu wamejaa wasiwasi, kulikuwa na watu wengi sana kule, na ndipo ikatendeka.

45 Juu ya Mlima wa Mizeituni kukaja maskini punda mweupe, akishuka chini ya kile kilima, huku kundi la watu likishangilia kwa fujo, wakikata majani ya mitende, wakitupa nguo zao barabarani, wakipiga makelele, "Hosana Mwana wa Daudi ajaye katika Jina la Bwana!" Yule . . . maskini nyumbu huyu, Mpandaji wake alikuwa si mwingine ila Masihi mpakwa mafuta wa Mungu kwa ajili ya wakati huo.

46 Mungu, wakati huo, alikuwa akifanya nini? Je, ni mvuto gani ulioko kwenye kile kilima? Ni Mungu akifanya historia, na Mungu akitimiza unabii. Na hiyo ndiyo daima inayosababisha kuvutia macho. Huwakusanya wapinzani wote, wale nderi (wa ujumbe wa asuhuhi hii), na tai pia. Unaona? Wanakusanyika pamoja kuona yanayotendeka. Baadhi yao wakija kwa uchunguzi, wengine wakija kutafuta makosa, baadhi yoa wakija kulaumu. Watu wa kila aina hukusanyika, kama tulivyosema asubuhi ya leo: waamini, wajifanyao waamini, na wasioamini. Kuna nini mlimani? Unabii unatimizwa. Sasa tutaona inayotendeka.

47 Sasa, katika Kitabu cha Zekaria, katika sura ya 9, na aya ya 9. Zekaria, mmoja wa manabii, alinena katika Roho, akisema haya:

*Furahini sana, Ee binti Sayuni;*

*Piga kelele, Ee binti Yerusalemu;*

*Tazama, mfalme wako amekufa kwako;*

*Ni mwenye haki, naye ana wokovu;*

*Ni mnyenyekevu, amepanda punda,*

*Naam, mwana-punda, mtoto wa punda.*

48 Sasa, walikuwa na nini wale waandishi? Walikuwa na nini wale makuhani? Walikuwa na nini wale watu wa dini? Haya yaliandikwa miaka mia nne na themanini na saba kabla hayajatendeka, kwa nabii aliyethibitishwa, na tayari yalikuwa yameandikwa na kuitwa Biblia, gombo la chuo cha Agano la Kale. Mbona hawangeliona ya kwamba huo ulikuwa unabii uliotimizwa? Kwa sababu ile ile hawawezi kuiona siku hizi.

Wamechukua Neno la Mungu na kulitangua mbele za watu, kwa kufundisha (kwa mapokeo) Mafundisho yaliyo maagizo ya wanadamu.

49 Na kama waandishi, wahubiri, wahudumu, watu wa rohoni (wanavyoitwa), wenye upako, wangesoma Biblia, hawangekuwa wakishangaa ni nini inayotendeka, wangejua ni nini. Mungu akitimiza Neno Lake!

50 Historia ilikuwa ikifanywa, unabii ulikuwa ukitimizwa. Wokovu kwa ulimwengu ulikuwa unawafikia, ile siku iliyo kuu ambayo manabii wote walikuwa wakiitazamia. Wote walio makaburini walikuwa wakingoja siku hiyo (Naam. Waza hilo!), wote waliokufa, wote wenye haki wa damu ya wafia imani na manabii.

51 Ambapo alikuwa tayari amepaza sauti, "Yerusalemu, Ee Yerusalemu, umuuaye kila nabii ninayemtuma kwako, na kuwaua wenye haki, ni mara ngapi ningekufunika kwa mabawa kama vile kuku kwa vifaranga vyake, lakini hukutaka! Bali sasa wakati wako umetimia."

52 Kila kitu kilichokuwa kaburini, Ibrahimu, Isaka, Yakobo, manabii wote, walingoja saa hii.

53 Nalo kanisa lilikuwa limepofuka Kwayo. "Ni nani huyu anayesababisha kelele hizi zote? Ni nani mtu huyu aliyesema wakati mmoja . . . Huyu si yule mwana wa seremala aliye humu? Tunamjua. Je, Yeye alipata hekima hii wapi? Naam, hatumwoni akihusiana na yo yote ya shule zetu? Hatujui vitabu vyo vyote alivyojifunzia? Je, huyu ni nani?"

54 Yeye alikuwa jibu la unabii wa nabii. Naye ndiye huyu akija, amepanda mwanapunda. Mvuto jinsi gani! Mungu alikuwa akitimiza Neno Lake lililoahidiwa, saa iliyokuwa ikingoja tangu miaka elfu nne. Katika Mwanzo, sura ya 3 na aya ya 15, Mungu alibashiri, "Mzao wa mwanamke utakiponda kichwa cha nyoka, bali kichwa chake kitakiponda kisigino chake," huo unabii kule kwenye Biblia uliokuwa umebashiri kuja kwa mtu huyu.

55 Na hapa hivi karibuni tu kulikuweko nabii aliyeinuka miongoni mwao, ambaye alithibitishwa nabii, Zekaria, naye akasema, ya kwamba, "Enyi binti za Yerusalemu nanyi binti za Zayuni, furahini, pazeni sauti, pigeni makelele, kwa maana mfalme wenu yuaja kwenu, mtiifu, mpole, mnyenyekevu, amepanda mwana-punda."

56 Na hapa wale watu ambao walisoma Maandiko hayo, siku baada ya siku, wakamtazama akiingia amepanda, na kulia, "Ni nani huyu?" Unaona? Mungu akitimiza Neno Lake kwa watu ambao iliwapasa kujua Ilikuwa nini, bali hawakujua.

57 Mungu anapotimiza Neno Lake, daima Inasababisha mvuto, kila mara hufanya hivyo. Husababisha mvuto fulani, kwa maana ni jambo lisilo la kawaida. Si la kawaida, anapotimiza Neno

Lake kwa wenye mtindo wa kisasa, kwa sababu watu wa kisasa hawaliamini. Wana njia zao.

58 Sasa, tunaona . . . Na turudie Maandiko na kuchukua baadhi ya matukio yasiyo ya kawaida, kwa dakika chache tu tena, ambapo Mungu alitimiza unabii Wake. Mungu anaposema kitu cho chote, Yeye atakitimiza. Mbingu zote na nchi zitapita, bali Neno haliwezi kupita kamwe. Kwa hivyo mara nyingi husababisha kioja, kioja kisicho cha kawaida.

59 Tazama jinsi Neno la Mungu lilivyo kama jambo la mzaha kwa wa—watu wanaotarajiwa kuliamini, walakini ni geni sana hata wanalia, "Vema, ni nini hii? Ulipata wapi upuzi huo? Ni nani huyu? Ni nini hii?" Wakati ingaliwapasa kupaza sauti kwa nguvu, "Hosana kwa Mfalme ajaye katika Jina la Bwana." (Bali kulikuwa kundi dogo tu lililokuwa likifanya hivyo, kundi dogo tu.) Kwa miaka elfu nne ya unabii, kwa jambo kubwa mno linaloweza kutendeka kwa taifa, kwa maana tumaini lote la waliokufa lilitegemea Hiyo, wakati wao wote wa usoni ulitegemea hayo, na wale watu wa dini waliodai eti waliiamini walikuwa wakipaza sauti zao, "Ni nani? Na tamasha hii ni ya nini?" Jambo geni! Ni vile vile, haibadiliki, sasa ni geni.

60 Hebu na tuone baadhi ya mambo mageni, kama nilivyosema. Je, nini kilichovutia macho kabla tu hukumu haijaupata ulimwengu na kuuangamiza kwa maji? Mzee, apataye umri wa miaka mia na ishirini, akijenga mtumbwi pasipokuwa na maji ya kuelea. Kule juu kwa miaka mingi, akisimama mlangoni, akijenga mle ndani, upande wa ndani, huku akiutia lami ndani na nje, na kusema, "Ulimwengu utamezwa na maji," katika wakati mkuu wa kisayansi.

61 "Je, ni nini kinachogongagonga kilimani kule juu?" "Naam, ni mzee jina lake Nuhu, naye yuko kule juu, mzee mkithiri dini. Huyu mzee alisimama juani muda mrefu zaidi, akapatwa na jua. Amerukwa na akili. Na anajenga anachoita 'safina,' na kusema maji yatatoka kule juu ambapo hamna maji, na yatawachukua watu wote humu, na kila mtu ambaye hatausikia ujumbe wake na kila mtu ambaye hataingia safinani atazamishwa. Je, mmepata kusikia jambo kama hilo?" Ulikuwa mvuto usio wa kawaida!

62 Nadhania, wale watu walipotaka kuangua kicheko, waliondoka wakaenda mbele ya mlango wa ile safina na kucheka. "Vipi, ulisema ingenyesha miaka mia moja iliyopita! Babu yangu aliniambia alikusikia huku juu ukisema ya kwamba itanyesha, nawe ungali unachonga-chonga kipande hiki cha mbao hapa. Mbona huwezi kujitambua mwenyewe?"

63 Bali ilikuwa Mungu akijitayarisha kuthibitisha ahadi na kutimiza unabii ambao nabii Wake alikuwa ametabiri. Jambo lisilo la kawaida kabisa! Mungu akitimiza ahadi Yake kwa Nuhu, huku wengine wakicheka. Mungu alikuwa pia

akijitayarisha kufanya historia kuonyesha wengine, hata leo, ya kwamba Yeye hutimiza Neno Lake! Haidhuru lisionekane kuwa la kweli jinsi gani, na lisilo na maana vipi, Yeye hata hivyo hutimiza Neno Lake. Yeye alikuwa akionyesha kwa mfano, kwa yule mzee aliyekuwa akigongagonga ile safina, kwa ajili ya watu hawa hapa Amerika usiku wa leo na ulimwenguni kote. Haidhuru sayansi inasema nini, wanayosema *(hili, lile,* na *linginelo),* Yeye hata hivyo hutimiza Neno Lake. Alikuwa akifanya historia.

64 Mvuto ulikuwa nini siku moja. . .Jambo lisilo la kawaida lilitendeka kule nyuma jangwani, na ilikuwa kijiti kilichowaka moto. Na nabii mtoro alikuwa amesimama kule chini jangwani. Hakusikia sauti kamwe, hakusikia mshindo wo wote, bali alitazama na kuona kitu kisicho cha kawaida kule juu mlimani. Mungu alikuwa akijaribu kuvutia usikivu wake. Ni vivyo hivyo leo!

65 Mungu alikuwa akijitarisha kutimiza Neno Lake, kwa nabii Wake Ibrahimu, "Uzao wako utakaa miaka mia nne katika nchi ya ugenini, nami nitawatoa kwa mkono wenye nguvu."

66 Naye alikuwa akimtayarishia mtu kazi hiyo, jinsi Yeye alivyokuwa akitayarisha safina kwa usalama wa wote ambao wangeamini. Mungu akawasha kijiti hiki, naye yule mchungaji, Musa, akasema, "Nitageuka tu nione jambo hili geni linamaanisha nini." Na alipomfanya Musa kukaribia kile kijiti, akamzungumzia.

67 Je, ule mvuto ulikuwa nini baadaye katika sebule ya Pilato, huyu Mchungaji alipokitupa kijiti chake chini na kikageuka kuwa nyoka? Mungu akitimiza ahadi yake kwa Musa. Je, ule mvuto kwenye Bahari ya Shamu ulikuwa nini, farasi za Farao zilipobubuazwa, walipoona upepo ukishuka kutoka mbinguni na kugawanya Bahari ya Shamu kutoka kulia hata kushoto; na maskini kundi la watumwa wakiwa wanaenda katika kazi ya Mungu wakavuka hiyo katika nchi kavu? Ilikuwa nini? Mungu akidumisha Neno Lake. Mauti yakaondoka, watu walio hai wakavuka; nao watu waliokufa kiroho wakajaribu kuiga hayo, nao wakazamishwa. Mungu akitimiza unabii na kufanya historia. Huo ndio ulikuwa mvuto kwenye Bahari ya Shamu.

68 Je, mvuto ulikuwa nini siku ya pili baada ya hayo kule kwenye Mlima Sinai, watu wote walipoagizwa wasiwakaribie wake zao, walipoulizwa waoshe nguo zao na kujitakasa wenyewe, na kukusanyika mlimani ambapo mtu fulani jina lake Musa alipokuwa amesema amekutana na Mungu katika Nguzo ya Moto? Naye Mungu akamwambia Musa, "Nitashuka miongoni mwa watu. Nitathibitisha yale niliyokwambia na Mimi ni Nani, nitawaonyesha ya kwamba Mimi ndiye Mungu yule." Hicho ndicho kilichovutia macho, Mungu akitimiza Neno Lake.

69 Nini kilichovutia siku moja katika historia, ambapo taifa fulani lilikuwa limemsahau Mungu, ambapo watu walikuwa wamekuwa baridi na wasiojali, ambapo makuhani wote walikuwa wameingilia mambo ya kisasa, manabii walitabiri kulingana na mapenzi ya makuhani? Na siku hizo, kama kawaida, walikuwa na mtu mmoja waliyemdhania kuwa mshupavu wa dini. Alinena kuhusu wanawake waliojipaka rangi, na kila kitu, naye alikuwa mtu wa kuchekesha. Naye mzee huyu alikuwa ameshuka na kumwambia mfalme "Hata umande hautaitwa . . . hautakuja hata nitakapouita."

70 Nasi tunatambua, basi, ya kwamba alikuwa amejificha na kulikimbia, naye alikuwa amejificha jangwani mahali fulani. Watu walidhani ya kwamba huenda ikawa amekufa kwa njaa ama ameangamia, bali alikuwa amelishwa vizuri sana, na kupewa maji, pia. Naye ndiye huyu hapa, akashuka na kusema, "Je, mmeona ya kwamba mimi nina BWANA ASEMA HIVI? Basi, kama hamjashawishika bado, hebu twendeni juu ya mlima tukathibitishe Mungu ni nani," kwa sababu alikuwa na ono lingine kutoka kwa Bwana.

71 Akasema, "Jichagulieni madhahabu, mkaitayarishe, na—na mkachague ng'ombe dume mkawachinje. Nitatengeneza madhabahu ya Bwana, nami pia nitamweka ng'ombe dume juu ya yangu. Nasi sote wawili tutatoa sadaka, na hebu na Mungu aliye Mungu ajibu." Yeye hangalitenda hayo iwapo Mungu hakuwa tayari amemwambia; alisema hivyo baadaye, "Nimefanya hivi kwa . . . yote haya kwa amri Yako, Bwana."

72 Bali mvuto ulikuwa nini? Mna makuhani mia nne waliosimama mlimani, naye mfalme yumo mle juu katika gari lake, pamoja na askari wake wote na walinzi waliomzunguka. Naye huyu mzee, mwenye nywele kama sufu, za kimbimbi, mwenye upara, na nywele zilizoning'inia usoni, amejizungushia kipande cha ngozi ya kondoo, nywele zimemjaa mwilini, huku amesimama na fimbo mkononi na chupa ya mafuta kwenye mkono mwingine, alikuwa amesema tu miaka mitatu na nusu hapo mbeleni, "Hata umande hautaanguka hata nitakapo . . . nitakapouagiza" (akichukua mahali pa Mungu, pamoja na vitu kama duara ya mwanga na vivuli na yote wanayonena habari zake). Na hapa yule mzee mshupavu wa dini amesimama mlimani, akiwapandisha watu hawa wote kule. Je, nini kilichowavutia? Ilikuwa ni Mungu akijitayarisha kuthibitisha nabii Wake kuwa ni wa kweli. Ilikuwa ni Mungu akitimiza unabii. Mungu pia akifanya historia, akitimiza Neno.

73 Miaka mia kadhaa baadaye, palikuweko mtu aliyekuwa na upako wa Roho yule yule, naye akajitokeza kutoka jangwani, hahusiki na madhehebu yo yote; ingawa baba yake alikuwa mtu wa dini, wa zamu fulani ya ukuhani. Bali akatokea jangwani, huku amevalia ngozi ya kondoo, huku nywele zimemjaa usoni mwake. Badala ya kuwa zenye mvi, zilikuwa nyeusi. Mtu huyu

alikuwa na mvuto gani uliowavutia Yerusalemu wote pamoja na Judea? Wengine walikuwa wakiondoka na kusema, "Kuna mshenzi kule chini, anajaribu kuwazamisha watu majini. Nani amepata kusikia jambo kama hilo?"

74 Wengine walikuwa wadadisi, wakisema, "Huyu hana budi kuwa Masihi." Mmoja akasema, "Huenda ikawa ni mmoja wa manabii." Hawakujua wawazie nini. Bali ilikuwa nini? Ilikuwa ni Mungu akitimiza Isaia 40, ambapo Yeye alisema, "Tazama . . ." yale angefanya siku za mwisho, jinsi angetuma mtumishi Wake na yale angetenda.

75 Ndipo tunaona, majuma machache baadaye, mtu huyo alikuwa hana shaka kabisa na ujumbe wake hata akasema, "Kuna Mmoja anayesimama miongoni mwenu Ambaye sistahili kuvaa viatu Vyake. Yeye atawabatiza kwa Roho Mtakatifu pamoja na moto, kama nilivyowabatiza kwa maji".

76 Na siku moja Kijana mmoja wa kawaida, mwenye umri wa kama miaka thelathini, akashuka na kubatizwa. Na mtu huyu alipokuja, yule nabii alivutiwa sana, huyo nabii akatenda yasiyo ya kawaida siku hiyo. Yale makutano hayangalijizuia kutazama matendo ya yule nabii alipokuwa akihojiana na makuhani upande wa pili wa mto.

77 Wao walisema, "Mungu alijenga madhebahu haya. Mungu ndiye aliyetuambia kufanya haya. Musa ndiye nabii. Tunamwamini Musa. Sadaka ya kuteketezwa haitaondolewa kamwe."

78 Naweza kumsikia Yohana akiwajibu, kasema, "Je, hamjasoma katika Maandiko yale Danieli nabii aliyosema, 'Sadaka ya kuteketezwa ya kila siku itaondolewa'? Na saa hiyo imefika sasa! Je, hamjasoma aliyosema Isaya katika sura ya 40, 'Sauti ya mtu aliaye nyikani, itengenezeni njia ya Bwana'? Hao ni manabii wawili kwangu. Na jambo lingine, je, ninyi hamkutambua nabii wetu miaka mia nne iliyopita, Malaki, aliponena katika sura ya 3 na kusema, Angalieni, namtuma mjumbe Wangu mbele Zangu kutengeneza njia yangu'? Je, hamjui ya kwamba hii inatimiza unabii?" Unabii ulikuwa ukitimizwa!

79 Na yapata wakati huo yule nabii akageuka akasema, "Tazama, yuaja pale Mwana-kondoo wa Mungu, aichukuaye dhambi ya ulimwengu!" Naam, ni mvuto gani? Ilibadilika kutoka kwa nabii hata kwa unabii wake.

80 Basi, angalieni iliyotendeka. Hapa yuaja mtu wa kawaida, hajulikani na ye yote, mwana wa seremala, akaja na kuingia majini. Ndipo Yohana, yule nabii mkuu, akasema, "Mimi nahitaji kubatizwa na Wewe. Nawe waja kwangu?"

81 Yeye akasema, "Kubali hivi sasa: bali kama nabii na Neno inatupasa kuitimiza haki yote."

82 Kwa hivyo akaelewa Dhabihu ilipaswa kuoshwa kabla haijatolewa, naye akambatiza.

83 Naam, kuna mvuto mwingine uliotokea Yeye alipotoka majini. Huyu nabii ambaye alikuwa mwaminifu sana kutangaza wakati wake na saa, alitazama juu na kuona mbingu zimefunguka, na akaona Roho wa Mungu, kama hua, akishuka juu Yake, na Sauti ikisema, "Huyu ni Mwanangu, mpendwa Wangu, ninayependezwa Naye." Mungu alikuwa akithibitisha ujumbe wa nabii, ndio ulikuwa mvuto kule Yordani.

84 Ndugu aliimba muda mfupi uliopita, ama alipaswa kuimba, *"Kilimani mbali sana mlisimama Msalaba wa kale unaoparuza."* Je, kuna mvuto gani juu ya Mlima Kalvari? Tunapoona kwamba ulimwengu wa kidini ulimhukumu, na serikali ya Kirumi ilikuwa imemhukumia kifo. Na hapa alikuwa amening'inia kati ya wahalifu wawili, akifa kwa kiu, Damu ikitiririka kutoka mwilini Mwake. Amening'inia pale, akilia, "Mungu Wangu, Mungu Wangu, mbona umeniacha?" Nao watu wa dini wamesimama pale wakiitazama, hawakujua ya kwamba unabii wa Agano la Kale ulikuwa ukitimilizwa pale pale Kalvari wakati huo.

85 Daudi mwenyewe aliandika, akatenda. . .akaingia katika Roho kama manabii wote, akatenda kama kwamba ilikuwa yeye. Daudi alilia katika Zaburi 22, "Mungu Wangu, Mungu Wangu, mbona umeniacha? Mifupa yangu yote imeteguka. Wamechoma mikono Yangu na miguu Yangu." Daudi akinena kama kwamba ilikuwa yeye. Na haikuwa Daudi, ilikuwa Kristo katika Daudi.

86 Na hapa unabii ule ule uliotolewa na wale manabii wote mbalimbali ulikuwa unatimizwa kwenye Mlima Kalvari. Je, kuna mvuto gani kwenye Mlima Kalvari? Mungu akitimiza Neno Lake.

87 Mvuto mwingine uliokuwa mlimani, ulikuwa kwenye Siku ya Pentekoste, wakati wote waliokuwa kule kwenye sikukuu ya kidini walidhania ya kwamba wameangamiza washupavu wa dini wote. Hawakuwa wamesikia habari zao kwa muda wa siku kumi. Mara tu, kama mzinga wa nyuki, wakatokea juu ya lile jengo, wakaingia barabarani, wakipiga makelele na kuendelea.

88 "Ni nini hii? Hii ina maana gani? Hawa watu wote wamelewa?"

89 Tazama! Na nabii akasimama miongoni mwao, jinsi taratibu za nabii zinapaswa kuwa, na akasema, "Enyi watu wa Uyahudi, na ninyi mkaao Yerusalemu na Judea, lijueni jambo hili, mkasikize maneno yangu. Watu hawa hawakulewa kama mnavyodhani wamelewa. Lakini jambo hili ni lile lililonenwa na Bwana kwa Yoeli, nabii, 'Itakuwa siku za mwisho, nitamwagia watu wote Roho Yangu." Huo ndio uliokuwa mvuto.

90 Watu wa dini, baada ya kumsulubisha yule Mkuu wa Uzima, na kila kitu, bado hawakuona ile ahadi ya kuja kwa

Roho Mtakatifu. Mvuto, "Ni nani huyu? Hii ina maana gani? Imekuwaje kwa watu hawa?"

91 Jamani! Ni vile vile leo. Tutapita mambo mengi kusudi tukailete kwa saa hii. Ni vile vile leo. Jambo lile lile linatendeka, maswali yale yale yanaulizwa, "Ghasia hizo zote ni za nini?" Angalieni huku na kule barabarani, motokaa kutoka Michigan hata Florida, kutoka Maine hata California. Asubuhi ya leo nilipokuwa nikiondoka, ama alasiri tulipokuwa tukitelemka barabarani, mimi na mke wangu tulikuwa tukichunguza leseni za motokaa. Hapo ndipo niliwaza juu ya somo hili.

"Je, hii ina maana gani?"

92 Kama lilivyosema tu, "Palipo mzoga, hapo watakusanyika tai"!

93 Nikamwambia mke wangu, "Mpenzi, unakumbuka usiku uliopita wakati ilinilazimu kuagana na kila kitu nilichokipenda duniani, na kuenda kule nje kuanzisha kitu ambacho Mungu alisema nifanye? Uliimba ule wimbo."

> Loo, watatoka Mashariki na Magharibi,
> Wametoka nchi za mbali.
> Kula pamoja na Mfalme wetu, wamekaribishwa chakulani kama wageni Wake;
> Jinsi wasafiri hawa walivyobarikiwa!
> Wanapouangalia uso Wake mbarikiwa
> Unaometameta kwa upendo wa kiungu;
> Ni washiriki wabarikiwa wa neema Yake,
> Watakaometameta kama johari katika taji Yake.

94 Huo ndio mvuto. Uzao wa Mungu uliochaguliwa tangu asili ambao hawawezi kutenda cho chote bali kulifuata, ni zaidi ya maisha kwetu. Twaa maisha yetu, bali usichukue Huo. Je, ni mvuto gani? Mungu, kama kawaida, akitimiza Neno Lake. Yeye yuatimiza Neno la Zekaria tena, nabii Zakaria.

95 Ambapo nilisoma aya ya 9 muda mfupi uliopita, wakati Yesu aliingia katika hekalu Lake, amepanda...ama akaingia Yerusalemu, akipanda maskini punda mweupe, unabii ulitimizwa ambao Zekaria alisema, uko hapa, "Furahini sana, Ee binti Zayuni. Shangilieni, Ee binti Yerusalemu. Tazama, Mfalme wenu anakufa kwenu, ni mwenye haki, Naye ana wokovu; ni mnyenyekevu, amepanda punda, naam, mwana-punda, mtoto wa punda." Huo ndio ulikuwa mvuto kule Yerusalemu, kwenye makao makuu ya kidini.

96 Sasa tunaona kituko cha siku za mwisho! Hebu na tufungue kurasa chache, katika Zekaria, na tuone aliyosema juu yake. Hebu na tufungue kwa ajili ya siku za mwisho. Hizo zilikuwa zamani za miaka ya katikati; hebu na tugeukie nyakati za mwisho. Na tufungue Zekaria, sura ya 14, tukianzia kwenye

aya ya 4. Na sikilizeni! Nasi tutasoma kipande cha Maandiko, kama vifungu tisa hivi, kutoka 4 hata 9. Sikizeni kwa makini. Nayo inatabiri juu ya Kuja Kwake, nyakati za mwisho, kwa hivyo sikizeni kwa makini sasa. Hii ni BWANA ASEMA HIVI, Ni Maandiko. Zekaria 14. Mnakumbuka Zekaria 9, ilivyosema? Nao hawakuitambua. Basi, vipi siku hizi? Zekaria 14, ikinena kuhusu Kuja Kwake:

> *Na siku hiyo miguu yake itasimama juu ya mlima wa Mizeituni* tena, *Yerusalemu upande wa mashariki, nao mlima wa Mizeituni utapasuka katikati yake, upande wa mashariki na upande wa magharibi; litakuwa huko bonde kubwa sana;. . .nusu ya mlima ule utaondoka kwenda upande wa kaskazini, na nusu. . .*kwenda *upande wa kusini.*

> *Nanyi mtakimbia kwa njia ya bonde la* mlima*; kwa maana bonde lile la* mlima *litaenea kutoka Aseli; naam, mtakimbia, kama vile mlivyokimbia* katika siku za *tetemeko la nchi, siku za Uzia, mfalme wa Yuda:. . .*

97 Tetemeko lingine la nchi litakalopasua nchi! Kama unataka kufuatilia Maandiko hapa, tazama katika aya hii ya 5, inanena kwamba kupasuka kwa Mlima wa Mizeituni kunasababishwa na tetemeko la nchi, na hii inathibitishwa na Isaiah 29:6 na Ufunuo 16:9. Kabisa! Ni nini? Nabii yule yule aliyeona kule kuja Kwake kwa kwanza, aliona Kuja Kwake kwa pili! Tazama, "Kama katika zile siku za tetemeko la nchi." Mnaona vile matetemeko ya nchi yanavyotenda, mnaona kubashiriwa kwayo?

> *. . .na BWANA, Mungu wenu, atakuja, na watakatifu wote pamoja naye.*

> *Tena itakuwa siku hiyo,* (Haleluya!) *katika siku hiyo, ya kwamba nuru yake haitakuwa na mwangaza au kiwi;*

> *Lakini itakuwa siku moja, iliyo. . .siku moja, iliyojulikana na BWANA: si mchana wala si usiku; lakini itakuwa, ya kwamba wakati wa jioni kutakuweko nuru.* (Ee Mungu!)

98 "Itakuwako Nuru yapata wakati wa jioni," nabii yule yule. Na watu ni vipofu! Je, ni nini kinachovutia? Hebu na tusome vifungu vingine vichache:

> *Tena itakuwa siku hiyo, ya kwamba maji yaliyo hai yatatoka Yerusalemu; nusu yake itakwenda upande wa bahari ya mashariki, na nusu yake. . .*kuelekea *upande wa bahari ya magharibi; wakati wa hari na. . .wakati wa baridi itakuwa hivi.* (Injili ikienda kwa Wayahudi na Mataifa wote wawili)

> *Naye BWANA atakuwa Mfalme juu. . .ya nchi: siku hiyo BWANA atakuwa mmoja, na jina lake moja.*

Itakuwa Nuru yapata wakati wa jioni, (sawa!)
Njia ya Utukufuni hakika utaipata;
Njia ya majini, ndiyo Nuru siku hizi,
Ukizikwa katika Jina la dhamani la Yesu.

Vijana kwa wazee, tumbuni dhambi zenu zote,
Roho Mtakatifu hakika ataingia;
Ile Nuru ya jioni imekuja,
Ukweli ni kwamba Mungu na Kristo ni mmoja.

Mnaona mahali tulipo?

Mataifa yavunjika; Israeli inaamka;
Ishara walizotabiri manabii wetu; (lile tetemeko la nchi kwa Mataifa siku za mwisho)
Siku za mataifa zimehesabiwa, zilizolemewa na hofu;
Rudini makwenu, Enyi mliotawanyika.

99 Ninyi mliofukuzwa, na sanduku hizi zilizobebwa katika magari mapya, tokeni huko kabla mauti hayajawapata. Mungu amelithibitisha. Itakuwa hivyo.

100 Hebu na tugeukie Andiko lingine katika Agano la Kale, Malaki, sura ya 4, na tusome hiyo sura ndogo ya 4.

> *. . . Angalieni, siku inakuja, inawaka kama tanuru; na watu wote wenye kiburi, nao . . . hao wote watendao uovu, watakuwa kama* makapi: . . .

101 Naam, hii si . . . hiyo ni Malaki 3 iliyokuwa kule kuja kwa kwanza, sasa huku ndiko kule kuja kwa pili. Hata Daktari Scofield hapa, hakika sikubaliani na maelezo yake, bali ameyaeleza hapa vizuri; agizo la Yohana, kwa Malaki 3; na kule Kuja kwa Pili kwa Kristo, na kwa Eliya hapo mbeleni.

> . . . watu wote wenye kiburi watachomwa moto, *asema Bwana wa majeshi; na haitawaachia shina wala tawi.* (Iko wapi jehanamu ya "Milele" basi?)
>
> *Lakini kwenu ninyi mnaolicha jina langu, jua la haki litawazukia, lenye* kampeni za uponyaji*, kuponya katika mbawa zake; . . . nanyi mtatoka nje, na kucheza-cheza kama ndama wa mazizini.*
>
> *Nanyi mtawakanyaga waovu, . . . watakuwa majivu chini ya nyayo za miguu yenu; katika siku ile niifanyayo, asema Bwana wa majeshi.*
>
> *Kumbukeni . . . torati ya Musa, mtumishi wangu, niliyomwamuru . . . huko Horebu kwa ajili ya Israeli wote, . . . amri na* hukumu.

102 Hapa kuna kule kuja kwa Eliya:

> *Angalieni, nitawapelekea Eliya nabii . . .*

103 Maandiko ya mwisho yanayomalizia Agano la Kale:

> . . .*Nitawapelekea Eliya nabii, kabla haijaja siku ile ya BWANA, iliyo kuu na ya kuogofya:*

104 Naam, huyo hangalikuwa Yohana. Sivyo. Tazama, ulimwengu haukuchomwa moto na watakatifu kuwakanyaga waovu. Mwaona? La, la.

> . . .kabla *haijaja siku ile ya BWANA, iliyo kuu na ya kuogofya.*
>
> *Naye ataigeuza mioyo ya baba iwaelekee watoto wao, na mioyo ya watoto iwaelekee baba zao, ili nisije nikaipiga dunia kwa laana.*

105 Tazama usahihi wa Roho Mtakatifu, ya kwamba haingeweza kutatanisha kule kuja kuwili kwa Eliya. Malaki 3, ilisema, "Angalieni, namtuma mjumbe Wangu mbele Yangu." Yesu aliulizwa habari za Yohana, Akasema, "Ikiwa tunataka kukubali, huyu ndiye manabii waliyesema, 'Nitamtuma mjumbe Wangu mbele Yangu.' Huyu ndiye Eliya atakayekuja." Malaki 3.

106 Tazama Maandiko yanatupa hilo kwa usahihi sana. Tazama vile hili. . .kuonyesha yale. . .wale wanaotaka kuamini, wale wanaotaka kuona. Kumbuka Yesu alikoma katikati ya Andiko, kwa sababu sehemu yake ilitimizwa wakati huo, iliyobaki ni ya Kuja Kwake kwa Pili? "Kutangaza mwaka wa Bwana uliokubaliwa, kuwaganga waliovunjika moyo", kisha akakoma; si "kuleta hukumu juu ya Mataifa" hata Kuja Kwake mara ya Pili.

107 Tazama Maandiko haya hapa yanakwenda sambamba na hayo. "Naye, Eliya, ataigeuza mioyo ya baba iwaelekee watoto wao." (Sasa, tukinena kuhusu Malaki 4, usiichanganye, ama Malaki 3.) Yohana, Eliya, aliyekuja katika zile siku kabla kule kuja kwa Kristo mara ya Kwanza, aligeuza mioyo ya wale wazee wetu wa kale kuelekea ujumbe wa watoto wao, ujumbe mpya.

108 Sasa tazama! "Na mioyo ya watoto iwaelekee baba zao." Katika kuja kwake mara ya pili, katika siku za mwisho, anawageuza kuwaelekezea imani ya kimitume tena. Wana vile Maandiko yanaambatana kikamilifu?

109 Huo ulikuwa ndio mwisho wa Agano la Kale, Agano la Kale. Sasa tunaona kuna Nuru wakati wa jioni. Ni nini? Ni kilele, mlima wa Kilele cha Mti.

110 Kama nilivyosema asubuhi ya leo, tumepitia kwenye madhehebu, kwenye (si mchungwa) kama nilivyosema asubuhi ya leo, bali tayari tumekuwa na zabibu, limau, namna ya vitu vingine vyote ambavyo havikuwa hivyo kamwe tangu mwanzo. Bali baada. . .Usilikose! Hapa laja! Baada ya madhehebu kumalizika, hayakuwa na Nuru kwanza, kutakuweko siku ambayo haiwezi kuitwa mchana wala usiku.

111 Je, wanafanya nini? Wanafanya nini? Je, li—limau hufanya nini kwenye mchungwa? Hutwaa uhai asili wa mchungwa

unaopanda juu na kuupotosha kuwa wa limau. Hivyo ndivyo madhehebu yamefanya kwa Neno la Mungu, yamelitangua Neno la Mungu kwa mapokeo yao. Hiyo ni ROHO WA BWANA ASEMA HIVI! Wamezaa malimau, mabalungi, si machungwa.

112 Bali nabii alisemaje? Yule yule aliyesema katika somo letu usiku wa leo, "Furahi, Ee binti Yerusalemu, shangilia kwa sauti kuu, binti Zayuni, kwa maana Mfalme wako anakuja kwako, mpole na mnyenyekevu, amepanda mwana-punda, mtoto wa punda," tazama ya kwamba nabii yule yule alisema, "Kutakuja wakati wa kuivisha." Jua limetumwa duniani kuivisha matunda. Mbona halikuweza kuivisha? Hamna tunda mle kuivishwa. Bali Uhai ungali unaendelea.

113 Ilifikia wakati wa balungi kuwa chungwa, tukapata kwamba ilifanyika dhehebu, ilikuwa balungi. Ikaendelea tena, ikawa kwamba ni limau. Ikaendelea tena, ikabadilika kuwa kitu kingine. Na mwishowe, juu ya mti ikageuka kuwa tunda la tangelo, ambalo ni nusu chungwa na nusu limau; uzao uliochanganyikana; kitu kilichopotoshwa, ikafikia upotovu, likiishi kwa mti ule ule; kapi, "nusura iwapotezea walio Wateule." Inaonekana kama chungwa, bali sivyo.

114 "Bali kutakuweko Nuru," linapositawi kushinda madhehebu. Linapopita madhehebu na kusitawi tena, litazaa machungwa kama lilivyokuwa lilipoingia ardhini. Na ndipo kutakuweko Nuru!

115 Nini hiki kinachovutia macho, ni nini kinachotendeka? Kutimiza Neno la Mungu! Kuna mashahidi wawili wa Agano la Kale, ya kwamba hii itatendeka.

116 Na tuchukue Yohana 14:12, ya Agano Jipya, Yesu alisema:

> . . . *Yeye aniaminiye Mimi, kazi nizifanyazo Mimi, yeye naye atazifanya;* . . .

117 Pia katika Luka 17:22 hata 30, Yeye alisema:

> Kama ilivyokuwa siku za Lutu, kabla Sodoma haijachomwa moto, *hivyo ndivyo itakavyokuwa Mwana wa Adamu* atakaporudi, *siku ile Mwana wa Adamu* anapofunuliwa.

118 Jamani, hebu chunguzeni tu Maandiko! "Mwana wa Adamu," Yesu Kristo yeye yule jana na hata milele, alikua akapita madhehebu, akakua akafikia kilele cha mti. Yeye alisemaje katika Yohana 14, ama 15? "Kila tawi ndani yangu lisilozaa tunda, litakatiliwa mbali na kukatwa, likatupwa motoni na kuchomwa. Bali kila tawi litakalozaa tunda, litatakaswa."

119 Naam, kutakuweko mvua ya kweli ya masika na ya vuli katika siku za mwisho juu ya hilo kundi dogo lililoambatana Naye alipopanda maskini punda yule, nyenyekevu na pole, lisilo na mashaka wala dhehebu, likilia, "Hosana, Mfalame ajaye

katika Jina la Bwana!" Kuna nini leo? Kuna mvuto gani kule mlimani?

120 Si muda mrefu uliopita, nikisimama kwenye mimbara hii, ilisemwa na Roho Mtakatifu, "Siku itakuja ambapo watapigilia kigingi mbele ya nyumba yako, wataliondoa lango lako. Kwa hivyo, hayo, hutayajali na usikasirike." Niliona lango langu limevujiliwa mbali na kutupiliwa kilimani. Niliona kile kilima mbele zangu kimelimwa chote, mbao na vinginevyo vilikuwa kule ambako mtu fulani alivivunjilia mbali. Akasema. . .Nikatazama, na alikuweko Jambazi aliyeenda kule na kuvunja-vunja lile lango, akatenda hili. Nikasema, "Mbona haukuniambia?" Akaanza ubushi hata ikanilazimu kumpiga. Na nilipofanya hivyo, nikasema, "Sijafanya hivi tangu nilipokuwa mwanandondi, bali nataka tu kujua," nami nikampiga konde moja. Na nilipomwangusha chini, nikamwinua tena na kumwangusha tena kwa ngumi. Nami nikamwinua mara tatu nne, na ndipo nikampiga na kumtupa upande mwingine wa kilima kile. Kwa hivyo nikaenda kule, nikasema, "Hiyo si sahihi." Nami nikamwinua na kumwamkua kwa mkono, nikasema, "Sikukasirikii, bali nataka ujue ya kwamba huwezi kunizungumzia hivyo." Na ndipo nilipogeuka na kurudi, Roho Mtakatifu alikuwa amesimama pale langoni, kasema, "Sasa usijali haya, kigingi hicho kitakapopigiliwa, geuka ushuke kwenda upande wa magharibi."

> Kitabu hiki ndicho cho chote ninachohitaji.
> Kitabu hiki kina Maelezo mazuri, (yanayoonyesha jinsi ninavyoweza kuepuka shida yangu)

121 Na ndipo Kitabu hicho ni Neno, na Neno hilo ni Mungu. Usijali shida zako, kitakwambia utakayofanya.

122 Miaka mitatu iliyopita nilimsikia rafiki yangu, bwana mpima mji, anaishi upande mwingine wa barabara kutoka kwangu, akipigilia kigingi. Nikatoka nje kule na kusema, "Kuna nini, Mud?" Mwanawe Bw. King, rafiki msiri wangu.

Kasema, "Billy, wanataka kuipanua barabara hii."

123 Nyote mnakumbuka? Nikasema, "Huenda ikawa ni ile daraja." Nikamwarifu Ndugu Wood, nikasema, "Shikilia mali yako. Huenda ikawa ile daraja itapitia hapa, ama cho chote kile." Kile kijia kilimbomolewa kabisa, matofali, miamba ilivurugiwa kila kitu. Kwa hivyo akasema. . .nikasema, "Shikilia mali yako."

124 Na ndipo nilipo. . .Bw. King akaniambia hiyo itatendeka, nikaingia na kumwambia mke wangu aliyeketi pale, "Mpenzi, kuna jambo lililoandikwa kuhusu hayo. Ni BWANA ASEMA HIVI, mahali fulani."

125 Nikaingia na kutwaa kitabu changu, nikakisoma, ilisema, "Itakuwa. . . " Miaka minane baadaye!

126 Na ndipo nilipokitazama, nikasema, “Wakati umewadia sasa, mpenzi, hatuna budi kwenda magharibi.”

127 Siku mbili baadaye nilipokuwa nimesimama chumbani yapata saa nne asubuhi, nikaingia katika Roho wa Mungu, nami nikaona lile kundi ndogo la huwa likipuruka, nikawatazama hao ndege wadogo. Mnakumbuka hilo. Nikawaona Malaika mfano wa piramidi, wakinijia kasi sana, kasema, “Geuka magharibi, nenda kule Tuscon, uwe maili arobaini kaskazini mashariki. Nawe utakuwa ukijitoa gugu fulani” (ama, huitwa kichwa cha fahari) “kutoka nguoni mwako.”

128 Ndugu Fred Sothman, anayeketi kule akinitazama sasa, alikuwa huko asubuhi hiyo. Nilisahau hayo.

129 Nikasema, “Mlipuko ulilipuka kama tetemeko la nchi ambao ulitikisa karibu kila kitu nchini. Sijui jinsi mtu angaliustahimili.” Nilishikwa na woga. Nilisimama kule Phoenix, nyote mnaosikiza usiku wa leo nishuhudieni. Nilihubiri mahubiri, *Mabwana, ni Wakati Gani?* “Tuko wapi?” Nikaondoka kwenda magharibi. Wengi wenu mna hiyo kanda, wengi wenu hapa mlisikia ikisemwa mwaka mmoja au zaidi kabla haijatendeka.

130 Niliondoka kwenda Magharibi, nikishangaa itakuwaje. Siku moja nikapata mwito kutoka kwa Bwana. Nikamwambia mke wangu, nikasema, “Mpenzi, huenda ikawa kazi yangu imekwisha.” Sikujua. Nikasema, “Huenda ikawa Mungu amemaliza nami sasa na nitakwenda Nyumbani. Mchukue Billy, ukawatuze watoto, Mungu atawasaidia, kwa vyo vyote vile. Enendeni mkaishi waaminifu kwa Mungu. Hakikisha ya kwamba watoto watamaliza masomo, ukawalee kwa maonyo ya Mungu.”

Yeye akasema, “Bill, hujui—hujui kama hiyo ni kweli.”

Nikasema, “La. Bali mtu hangaliweza kustahimili huo.”

131 Na asubuhi moja Bwana aliniamsha, kasema, “Nenda kule juu kwenye Magenge Marefu ya Sabino.” Nami nikachukua kipande cha karatasi pamoja na Biblia yangu.

Mke wangu akasema, “Unaenda wapi?”

Nikasema, “Sijui. Nitakuambia nitakaporudi.”

132 Nikakwea yale magenge, nikapanda mpaka kule juu kabisa tai walikokuwa wakipuruka huku na huko. Nilikuwa nikiwatazama baadhi ya kulungu waliosimama kule. Nikapiga magoti kuomba, nikainua mikono yangu, na Upanga ukauangukia mkono wangu. Nikageuka nikawazia, “Nini hiyo? Sijapatwa na kichaa. Hapa mna ule Upanga mkononi mwangu, unaong’aa, unanawiri, unametameta juani.” Nikasema, “Naam. Hamna watu kwa maili nyingi kutoka hapa nilipo kwenye magenge haya. Je, huo ungetoka wapi?”

Nikasikia Sauti, kasema, "Huo ndio ule Upanga wa Mfalme."

Nikasema, "Mfalme ye yote humpandisha mtu cheo kwa upanga."

133 Yeye yule Sauti akarudi, kasema, "Si upanga wa mfalme," bali 'ULE Upanga wa Mfalme,' Neno la Bwana." Kasema, "Usiogope, ni ule Mvuto wa Tatu tu. Ni thibitisho la huduma yako."

134 Nilikuwa nikienda mawindoni pamoja na rafiki yangu, bila kujua itakayotendeka. Na mtu fulani akanipigia simu, ambaye alinilaumu kwa ajili ya ile picha ya Malaika wa Bwana, ambayo aliipiga. Ilinilazimu kwenda Houston kwa ajili ya mwanawe, kwa maana alikuwa akielekea kwenye maangamizi naye angekufa katika muda wa siku chache. Naye akakutana nami kule ndani na kunikumbatia kwa mikono yake, kasema, "Waza, mtu yule yule niliyemlaumu amekuja kuokoa mwanangu wa pekee!" Chama cha masilahi ya binadamu kikanitunza nishani inayoitwa Oscar, ama cho chote unachotaka kuiita, kwa ajili ya kuokoa maisha.

135 Ndipo tukarudi, nikapanda mlimani kwenda mawindoni. Na hapo Ndugu Fred na mimi, asubuhi moja nilipoondoka, tayari nilikuwa nimempata javelina wangu, na nikatazama na kuona mahali alipokwenda. Nikasema, "Ndugu Fred, panda mlima ule asubuhi na mapema sasa, kwenye mapambazuko, nami nitapanda ule mwingine. Sitampiga risasi yule nguruwe mwitu, sitamuua. Bali wakianzia upande huu, lile kundi, nitapiga risasi mbele yao kuwarudisha nyuma."

136 Ndugu Fred akaenda kule na hakukuwa na nguruwe mwitu. Akanipungia mkono nami nikamwona. Nikatelemka katika yale magenge, mashimo makubwa sana, jua lilikuwa likichomoza. Nikazunguka upande mwingine wa kile kilima, bila kufikiria cho chote juu ya ule unabii. Nikaketi chini, nikingoja, nikipumzika, nikawazia, "Imekuwaje kwa wale nguruwe mwitu?"

137 Nami nikatwaa. . .Nikaketi jinsi Wahindi huketi, mwajua, kupitanisha miguu, nami nikaangalia mguu wa ovaroli yangu na ilikuwa na mbegu ya kwekwe. Nikaitoa, na kusema, "Hiyo ni ajabu! Niko hapa, yapata maili arobaini kaskazini mashariki ya Tucson. Huyo ni mwanangu mdogo Joseph ameketi kule akiningojea." Na mara nilipoanza kutazama, nikaona kundi la nguruwe mwitu yapata yadi elfu moja kutoka kwangu, juu mlimani, nami nikatupa ile mbegu ya kwekwe chini. Nikasema, "Nitawapata. Nitaenda nikamwite Ndugu Fred, nami nitatundika kipande cha karatasi kutujulisha tupitie wapi kwenye mzingile mwanambije huu hapa, nasi tutampata Ndugu Fred."

138 Nami nikaanza kupanda ule mlima, huku nikikimbia sana nilivyoweza kando kando. Kwa ghafula, nilidhani mtu fulani alinipiga risasi. Sijapata kusikia mlipuko kama huo, ulitikisa nchi nzima. Na, ulipofanya hivyo, mbele zangu wakasimama Malaika saba katika kundi moja.

139 Nilikutana na Ndugu Fred muda kidogo baadaye. Kasema, "Ilikuwa nini?"

Nikasema, "Hiyo ilikuwa ndiyo."

"Utafanyaje?"

140 "Rudi nyumbani. Kwa maana BWANA ASEMA HIVI, zile siri saba ambazo zimefichwa katika Biblia miaka hii yote, madhehebu haya na kila kitu, Mungu atatufungulia zile siri saba katika zile Muhuri Saba."

141 Kulikuwa na ule mviringo uliokuwa ukitoka ardhini, kama ukungu. Ulipofanya hivyo, ukapanda moja kwa moja juu ya mlima kabisa, ukaanza kuzungukazunguka pande za magharibi jinsi ulivyokuja. Sayansi ikauona baada ya muda kidogo, maili thelathini kwenda juu na maili ishirini kutoka upande mmoja hata mwingine, kama mviringo wa piramidi hasa.

142 Na hivi majuzi, nilipokuwa nimesimama pale, nikaigeuza ile picha upande wa kulia, Yesu akaonekana mle jinsi alivyokuwa katika zile Nyakati Saba za Kanisa, mwenye kufunikwa nywele nyeupe, ikionyesha Uungu Mkuu. Yeye ni Alfa na Omega; Yeye ni wa Kwanza na wa Mwisho; Yeye ndiye Hakimu Mkuu wa Milele yote, aliyesimama pale, akathibitisha Ujumbe wa wakati huu. Na kutakuweko Nuru wakati wa jioni! Je, maana yake yote ni nini? Ilikuwa nini?

143 Nikaenda upande wa magharibi. Juu ya mlima ule ule, nikipita pale pamoja na Banks Wood pale, kasema, "Tupa jiwe hewani. Mwambie Bw. Wood, 'BWANA MUNGU AMESEMA HIVI, utaona Utukufu wa Mungu."

144 Siku iliyofuata, nikisimama pale, upepo wa kisulisuli ukashuka na kulipua mlima kabisa. Majabali yalikatilia mbali vilele vya miti, yapata futi tatu nne juu ya kichwa changu. Ukasababisha milipuko mitatu mikubwa, na ndugu wakanikimbilia. Kulikuwa yapata watu kumi na watano waliosimama pale, wahubiri na wengineo. "Kuna nini?" Yeye akasema, "Ilikuwa nini?"

Nikasema, "Hukumu unaijilia Pwani ya Magharibi."

145 Yapata siku mbili baadaye, tetemeko la nchi nusura lizamishe Alaska. Je, hii Nuru juu ya Mlima Sunset katika Msitu wa Coronado wa Arizona ni nini? Je, kitu hiki cha ajabu kilichotukia kule juu ambacho watu wamekuwa wakisafiri kuelekea mashariki wakitoka magharibi kuokota mawe yaliyotawanyika mle lilipolipuka, na kila moja yao, kila moja ya majabali hayo, lina ncha tatu, lilizopasua. (Watatu ni Mmoja)

Yamewekwa kwenye madawati, yanawekwa juu ya karatasi, kote nchini. Je, ni jambo gani hili la ajabu juu ya Mlima Sunset katika Msitu wa Coronado?

146 Junior Jackson unasikiza, je, unakumbuka ile ndoto aliyokuwa nayo ambayo niliifasiri, "kuelekea kwenye machweo ya jua"? Na hii ilitendeka kwenye Mlima "Sunset" (Machweo ya Jua)! Ni wakati wa jioni, wakati wa machweo. Ujumbe wa machweo kwa machweo ya historia, machweo ya unabii, hasa, ukitimizwa. Na kutakuweko Nuru wakati wa jioni juu ya Mlima Sunset katika Msitu wa Coronado, maili arobaini kaskazini mwa Tucson. Chukua ramani ukaone Kilele cha Sunset pale. Hapo ndipo hasa ilipotendeka. Sikujua hayo kamwe hata hivi majuzi.

147 Kila kitu, hiyo—hiyo haitakufa kamwe, inajifunua yenyewe daima. Kutoka kwa mambo yayo hayo yanayotendeka, hata kwa picha ya Yesu aliyesimama akituangalia, na sasa katika Mlima Sunset hasa, na Nuru ya machweo. Ile Nuru ya jioni imekuja, Mungu anajithibitisha Mwenyewe. Ni nini? Bila shaka Mungu na Kristo ni mmoja. Kile "cheupe." Wangapi wamepata kukiona, zile nywele nyeupe juu Yake, kama tulivyonena katika Ufunuo 1? Unaona, Uungu Mkuu sana, Mamlaka Makuu sana! Hamna sauti nyingine, hamna mungu mwingine, hamna kingine kile. "Katika Yeye mnakaa utimilifu wa Uungu kwa jinsi ya mwili." Malaika wenyewe ndio waliokuwa nywele nyeupe Zake. Amina.

148 Je, nini ilitendeka kwenye Mlima Sunset? Mungu akithibitisha Neno Lake. Hiyo ndiyo sababu ya kelele hizi zote. Tazama, ni Mungu akitimiza Neno Lake lililoahidiwa tena, la Ufunuo 10:1 hata 7, "Na katika siku za kupigwa baragumu ya Ujumbe wa malaika wa saba, hapo ndipo siri ya Mungu inapaswa kutimizwa." Ile siri iliyofichwa ya Ufunuo 10:1 hata 7, ule ujumbe wa mwisho kwa ajili ya wakati wa mwisho wa kanisa. Unatimiza kabisa, katika zamani hizi, Luka Mt. 17:30, "Siku atakapofunuliwa Mwana wa adamu."

149 "Na watainuka manabii wa uongo na makristo wa uongo, watakaoonyesha ishara kuu na maajabu, hata ingewapoteza, kama yamkini, walio wateule." Huku watu wangali wana shaka na, kama kawaida, kanisa nalo limetatanika vile vile.

150 Na sayansi kote katika Tucson, wangali wanaandika makala madogo madogo na kuyaweka magazetini. Kule nyuma mbali sana juu ya Mlima Lemmon, zile kamera kubwa hazikuiona ikiinuka kutoka mahali tulipokuwa tumesimama; ikipeperukia upande wa magharibi, ikionyesha ya kwamba wakati umekwisha. Haiwezi kusonga tena isipokuwa mahali padogo sana, iko kwenye Pwani ya Magharibi. Hukumu ilitokea tu jinsi ilivyoenda. Ikaenda juu kule kupita Phoenix na kuvuka ng'ambo moja kwa moja, hata Prescott na kuvuka milimani hata

Pwani ya Magharibi, moja kwa moja hata...Ilikuwa ikienda wapi? Kule juu mpaka Alaska, na inanguruma, ikielekea kule.

151 Na vituo vya uchunguzi wa angani na wengine wote kule Tucson wangali wanauliza, watafiti wa sayansi wanajaribu kuchunguza ni nini. Ilikuwa juu sana ambamo hakuwezi kupata ukungu, umande, ama cho chote kule. "Ilisababishwa na nini? Iko wapi?" Wao wametatanishwa vile vile na ile duara ya mbinguni inayoning'inia kule juu mbinguni kama walivyokuwa wale mamajusi walipokuja wakiifuata nyota, wakisema, "Yuko wapi aliyezaliwa Mfalme wa Wayahudi?" Ilikuwa nini? Mungu akitimiza Neno Lake, "Na nyota itatokea kwa Yakobo."

152 Naye Mungu wa Mbinguni aliahidi ya kwamba wakati wa jioni utakuwa na Nuru ya jioni. Miaka mitatu iliyopita siri hii ilikuwa unabii, "Je, ni wakati gani, bwana?" Bali sasa ni historia. Imepita. Ile ahadi imetimizwa. Ni wakati gani, bwana, na mvuto huu ni wa nini? Mungu akitimiza Neno Lake! Ni yeye yule jana, leo, na hata milele.

Na tuombeni:

153 Mungu mpendwa, nimewazuia watu hawa kwa muda, muda mrefu zaidi ya nilivyotarajia. Naomba, Mungu, ya kwamba jambo fulani lilisemwa ama kutendwa ambalo litawafanya watu kila mahali kuelewa. Na kwa kuona na kuelewa huenda wakaamini ya kwamba Wewe ndiye Kristo wa kweli, na Maneno ambayo yanathibitishwa ni thibitisho la Neno Lako kuwa kamilifu na kutimizwa katika wakati Wake.

154 Sasa, Bwana Yesu, kutoka kwa Maneno Yako Mwenyewe, ulisema ya kwamba ulimwengu ungekuwa katika hali ya Sodoma. Tunajua hayo, tunaweza kuutazama. Nawe ulisema, katika siku hiyo, "kama alivyokuwa katika Sodoma." Kulikuwako wajumbe watatu waliotumwa kwa ulimwengu wa Mataifa na Waebrania. Na mmoja wao, ambaye alikuwa Mungu Mwenyewe, Mwana wa Adamu, alijifunua Mwenyewe katika mfano wa mwanadamu na kufanya muujiza, hata akamwambia Ibrahimu yale Sara alikuwa akitenda nyuma Yake katika hema.

155 Ulisema ingejirudia tena wakati ulimwengu wote wa Mataifa utakuwa katika hali ya Sodoma. Na imekuwa hivyo, Bwana. Utabiri ule mwingine ukithibitisha jambo lile lile, kuhusu kutumwa kwa Eliya katika siku za mwisho, ile Roho ya Eliya juu ya nchi, kuleta mioyo ya baba, ama "ya watoto iwaelekee baba zao." Nami naomba, Mungu, ya kwamba saa hii utathibitisha Neno Lako, ya kwamba ni wewe yule jana, leo, na hata milele. Tujalie, Baba. Wao ni Wako. Naomba ya kwamba utatujalia baraka hizi na kuthibitisha yale ambayo yamenenwa, kwa ajili ya Utukufu wa Mungu. Katika Jina la Yesu Kristo. Amina.

156 Kunena neno, ni mtu; kuthibitisha neno, ni Mungu. Kusema neno, ni jambo moja; Mungu kulitimiza, ni lingine. Mungu hahitaji mfafanusi ye yote, Yeye hujifafanulia Mwenyewe.

157 Sasa tunakaribia kuwa na mstari wa maombi, kuwaombea wagonjwa, Mungu akitujalia. Nasi tunajua ya kwamba hamna ye yote, hamna mtu, si mwanamke, si binadamu, si malaika, anayeweza kukuponya, kwa maana Mungu tayari ametenda hayo. Yeye alishughulikia hayo, jambo tu linalokupasa kufanya ni kuyapokea.

158 Hamna mtu, si malaika, si cho chote kile, si hata Mungu Mwenyewe, awezaye kukusamehe dhambi zako. Hiyo imetendwa tayari. Yesu alifanya hayo Msalabani. Bali haitakufanikisha kitu, ama kukufaidi kitu, hata utakapoikubali. Unaona?

159 Jambo pekee liwezalo kufanywa, ni agizo ambalo limetolewa na Mungu, kwa waamini kuwekea wagonjwa mikono. Hiyo wamefanya katika nyakati zote, kwa ufufuo. Na wameita, "Mungu."

160 Ibrahimu aliona ishara nyingi. Bali kulifikia wakati ambao Ibrahimu aliona ishara yake ya mwisho, kabla tu Sodoma haijachomwa, na hiyo ilikuwa Mungu akijidhihirisha Mwenyewe katika mfano wa mwanadamu. Je, mnaamini hayo? Je, Yesu alisema ingejirudia?

161 Basi ni wangapi humu . . . Na kule nje redioni, ama huko simuni kote nchini, kama mngali mnasikiza, iweni tayari kwa maombi, iweni mkiomba, nanyi ambao mna leso hizi hapa. Naam, siwezi nikamwambia Mungu ya kutenda. La. Jambo hili na liwe mbali nami hata kujaribu. Yeye ni mwenyezi, hutenda anayotaka kutenda. Yangu tu ni kutii na kusema yale Yeye asemayo.

162 Na, sasa, wanasimama kote kutani, nao wamejazana na kusongamana. Nashangaa kama tungemuuliza Mungu tukitumia maneno haya, "Huu ni mvuto gani?" kama Mungu angetenda miongoni mwetu tena (huenda kuna wageni hapa), na kutenda miongoni mwetu na kuonyesha uso Wake mbarikiwa miongoni mwetu, akaonyesha Roho Wake hapa, akaonyeshe ya kwamba ni yeye yule jana, leo na hata milele, hata kila mmoja wetu (baada ya jumbe hizi mbili kali) apate kuamini ya kwamba ni kweli. Mngeweza kufanya hivyo? Naam basi.

163 Badala ya kuagiza mstari wa maombi basi, kuna joto, msongamano, kusimama kuegemea ukuta . . . Nikitazama huku kuagiza mstari wangu wa maombi, hamngeweza kuufanya kwa kusimama hapo. Je, ningeweza kuuagiza upande huu? Ninyi mlio wagonjwa, machela, kila kitu, mliolala, hamngaliweza kuufanya. Kwa hivyo ketini mlipo, na mkamwamini Mungu. Kama mna kadi ya maombi, ishikilieni, itafaa. Tutakufikieni kama tunataka kupitia katika mstari. Bali si lazima upitie mstarini.

164 Yule Bw. Shepherd, jumapili iliyopita, hakupitia kwenye mstari wo wote. Si—sidhani alikuwa na kadi ya maombi. Je, Bw. Shepherd yuko humu usiku wa leo? Yuko wapi? Yuko hapa? Yuko kule nyuma. Ulikuwa na kadi ya maombi, Bw. Shepherd? Hukuwa nayo? Hakuwa nayo. Yeye ameketi pale pale tena usiku huu. Hapo ni mahali pazuri kuwepo, Ndugu Shepherd.

165 Siyo tu muwe pale, bali iweni na imani tu. Kwa maana, kumbukeni, maskini mwanamke mmoja aligusa vasi Lake Naye akasikia hilo. Naye ni yeye yule jana, leo, na hata milele. Na waraka wa Waebrania, katika Agano Jipya, ulisema ya kwamba Yeye ni "Kuhani Mkuu" usiku wa leo anayeweza "kuchukuana nawe katika mambo yako ya udhaifu." Je, mnaamini hayo? Basi iweni na imani! Msilitilie shaka. Aminini, na itatendeka. Mnaweza kupata yale—yale mmeomba, kama mnaweza kuiamini. Bali hauna budi kuamini. Mtafanya hivyo? Ninyi nyote mtaamini? Je, wangapi mtaiamini sasa? Mungu awabariki!

166 Sijui nani ni nani, simjui ye yote wenu. Si kazi yangu kujua ye yote wenu, ni kazi ya Mungu kujua mambo haya. Bali atatenda haya kama mtaamini. Mtaamini sasa?

167 Sasa, Mungu mpendwa, bila shaka huna kundi la Wakristo waliochanganyikana, haitupasi kuwa watu ambao inawapasa kubembelezwa na kuendekezwa kitoto. Wewe huna watu wa aina hiyo, Bwana. Una waamini waliokomaa. Uwepo halisi wa Mungu huiwasha moto mioyo yao. Kama Ibrahimu, alimwamini Mungu. Ulijijulisha kwake, ndipo Wewe ukaja kwake na kufanya ishara, naye akakuamini. Ukabadilisha mwili wake kurudia ujana, na pia mkewe, ambaye, mkewe alikuwa sehemu ya mwili wake mwenyewe. Ndipo akazaliwa yule mtoto mpya, mwana aliyeahidiwa.

168 Mungu, uliahidi ingekuwa jambo lile lile kwenye siku hii. Naomba ya kwamba Wewe utathibitisha Neno hili. Nasi tutashughulikia moja kwa moja ahadi hiyo moja pale, ya kwamba itakuwa kama ilivyokuwa Sodoma, kabla tu Sodoma haijachomwa moto na hukumu ikaikalia Sodoma, ulimwengu wa Mataifa. Kwa hivyo hukumu inakaribia kuuangukia ulimwengu wa Mataifa, nao Wayahudi wana miaka mitatu na nusu zaidi kupitia wakati wa Dhiki, taabu yake Yakobo, kuendelea kwa majuma sabini ya Danieli. Bali majira ya Mataifa yamehesabiwa, ni wakati wa kuondoka. Nawe ulitoa ishara hiyo, na ukasema ya kwamba itakuweko tena. Tujalie Mungu. Yao . . . tumo mikononi Mwako, tufanyie unayoona yanafaa. Katika Jina la Kristo. Amina.

169 Naam, msiwe na wasiwasi. Ingekuwaje kama nilikuwa na wasiwasi? Sasa, nafanya jambo hapa ambalo halina budi kutegemea mamlaka ya Mungu. Bali mbona ninafanya hivi? Yeye alisema itakuwa hivi. Hiyo yatosha. Na kama akijithibitisha

Mwenyewe hivyo mbele zenu, vema, hamuwezi kumwamini? Bila shaka. Ninyi iweni na imani tu sasa na muamini. Na hebu nitazame huku na huko, nikaone ambapo Roho Mtakatifu ataongoza, yale atakayotenda. Sijui atakayotenda, hiyo ni juu Yake. Bali kama nitakuwa tu na imani, mkaamini tu, "mambo yote yawezekana kwao waaminio." Nyote mnaoamini hayo, inueni mikono yenu na kusema "Naiamini" [Makutano wanasema, "Naiamini. "—Mh.] Kwa moyo wako wote amini.

170 Basi, tatu itakuwa thibitisho, iwapo ataifanya mara tatu moja kwa moja kuwathibitishieni ya kwamba ni kweli. Sijali uko wapi, u nani, wewe uwe tu na imani ukaamini. Naam, msi—msijongee po pote.

171 Bibi, unayeomba, sikujui. Keti tu ulipo, haikupasi kuja. Sikujui, bali umemshika msichana mdogo mikononi mwako, au, pajani mwako. Mimi ni mgeni kabisa kwako. Na huyo msichana mdogo anaonekana mzima, aonekana mwenye nafuu. Yeye ni msichana mdogo mrembo, msichana mdogo mwenye nywele nyekundu. Nilimtazama hapa, haonekani kilema au cho chote kile. Sijui anaugua wapi. Huenda ikawa si kwa ajili ya mtoto huyo, huenda ikawa ni kwa ajili yako. Kwa bahati tu nilikuona umeketi pale pamoja na mtoto huyo, na ukiomba. Inanibidi kunena nawe kwa muda mdogo kusudi nipate roho yako, kama Yesu alivyomwambia yule mwanamke, "Nipe maji ninywe," unaona, kumchukua tu—kumchukua tu mtu mmoja. Ndugu Bryant na wengineo walioketi hapa, nawajua watu hawa walioketi hapa. Huenda wakawa wahitaji, pia, bali ulikuwa mgeni.

172 Je, unaniamini mimi kuwa nabii wa Mungu? Je, unaamini mambo haya ambayo umesikia usiku wa leo ni Kweli? Basi, kama Mungu atanifunulia jambo ambalo umetenda, ama jambo ambalo halikukupasa kutenda, ama kitu kibaya kwako, ama unayotaka, utajua kama ni kweli ama si kweli. Sivyo? Na iwapo atafanya hivyo, je, itathibitisha Neno Lake ya kwamba ni yeye yule jana, leo, na hata milele, na ya kwamba Luka Mt. 17:30 tayari inadhihirishwa? Je, unaiamini?

173 Naam, wewe bibi uliinua mkono wako ya kwamba sisi ni wageni. Sikujui, bali ninajaribu kupata roho yake, mtu mmoja. Wengi wenu wanavuta. Naam, amini haya kwa moyo wako wote. Basi, ni kwa ajili ya huyo msichana mdogo. Si wewe. Una wasiwasi, bali si huo wasiwasi unaokusumbua. Jambo kubwa moyoni mwako ni huyo msichana mdogo. Na unaamini Mungu anaweza kuniambia ni nini? Unaamini? Je, ingekusaidia, ungeamini basi? Ni jeruhi kwenye ubongo. Sivyo? Sasa, weka mkono wako kwenye kichwa cha mtoto huyo mchanga, mkono wako.

174 Mungu mpendwa, Wewe ulisema, "Ishara hizi zitafuatana na hao waaminio. Wataweka mikono yao juu ya wagonjwa, nao

watapona." Yule mwanamke ni mwamini. Mkono wake umo juu ya mtoto. Na apone. Katika Jina la Yesu Kristo, naomba sala hii. Amina.

175 Sasa, mnaamini, ninyi nyote? Ukiweza kuamini, yote yawezekana. Bila shaka!

176 Namjua bibi anayeketi pamoja naye, bali anatazama huku kwa unyenyekevu sana. Siwezi kuita jina lake, vema, kama ningemtazama kwa dakika moja ningejua. Bali namjua mwanamke huyu kwa uso, bali sijui shida yake ni nini? Unaamini mimi. . . Mungu atanijalia kujua shida yako ni nini? Unge. . . Ingekusaidia? Ugonjwa wa sukari. Basi, kama hiyo ni kweli, inua mkono wako. Bila shaka!

177 Imekuwa bibi anayelala. . . anayeketi karibu nawe ana jambo lile lile. Yeye ni mgeni. Yule bibi mwingine anamwombea mtu fulani, mtoto kiwete. Amini kwa moyo wako wote, Mungu atamjalia.

178 Mtu mwingine nyuma humu. Mtu yule anayeketi kule anajaribu kuacha kuvuta sigara. Je, unaamini ya kwamba Mungu ataziondoa kwako? Naam. Unaamini? Unaweza kuipokea. Sijapata kumwona mtu huyo maishani mwangu.

179 Hapa yuko mtu. Je, mnaona lile wingu jeusi linalonig'inia juu ya mtu huyu papa hapa ambaye amelala katika kitu kama machela, au kiti? Anakufa. Ametiwa uvuli, yuna kansa. Simjui mtu huyu, sijamwona kamwe. Mungu anajua yote juu yako. Hiyo ni kweli, bwana. Je, unaamini ya kwamba Mungu angeniambia neno juu yako? Ingekusaidia kupokea uponyaji wako? Ulileltwa humu na rafiki yako. Bali wewe si mwenyeji wa hapa, uko mahali ambapo pana maji mengi sana, wanakovua samaki. Naam, Albany, Kentucky. Hiyo ni kweli. Amini, unaweza kurudi nyumbani mwenye afya. Amini ya kwamba limeondoka. Kama utaamini! Huna budi kuamini! Lazima uamini, na uamini ya kwamba imetendeka kwako. Je, unaamini?

180 Wewe, kutoka Tennessee, una kijana aliye na ugonjwa wa pumu. Hayuko hapa, bali unaamini ya kwamba ataponywa? Basi mpelekee leso yako—mkononi mwako kwake. Ataponywa kama ukiiamini.

181 Huyo bibi anayelia, anayeketi upande mwingine karibu na Daktari Vayle pale. Ametiwa kivuli, pia, kivuli cheusi. Sijapata kumwona mwanamke huyo maishani mwangu, bali yuna kansa. Atakufa kama hatendewi kitu. Je, unaamini ya kwamba Yeye atakuponya, bibi? Unaweza? Unaweza kupokea uponyaji wako, kama ukiamini tu.

182 Kuna bibi mdogo anayeketi moja kwa moja nyuma yake mwenye leso kinywani mwake. Yeye pia ana tumbo lililo na vidonda, mgonjwa. Umekuwa ukizirai, kupofuka, kuzimia. Mtu fulani alikuleta hapa. Una shida za kike. Kama utaamini, unaweza kwenda nyumbani ukapone.

183 Wewe, kijana, ni mgeni, unayeketi papa hapa mbele zangu, ukinitazama. Wewe ni nani, M-Puerto Rico au nini? Naam, namaanisha. . .?. . .Mimi ni mgeni kwako, unajua hivyo, hata hutoki katika nchi yetu. Bali unaamini ya kwamba Mungu anaweza kukupa shauku ya moyo wako? Kama nitakwambia shauku yako ni nini, je, utaipokea? Unatafuta ubatizo wa Roho Mtakatifu. Hiyo ni kweli. Pokea Roho Mtakatifu, ndugu yangu.

184 Hapa kuna mtu mweusi ameketi huku nyuma kabisa, ana mzigo moyoni mwake, kwa ajili ya mkewe. Yeye hayuko hapa, hata. Anaugua miguuni. Unaamini ya kwamba Yeye atamponya? Unaamini? Wewe ni mgeni hapa. Umetoka ng'ambo. Umetoka Jamaica. Je, unaamini Mungu angeniambia wewe ni nani? Bw. Braden. Unaamini? Yesu Kristo ni yeye yule jana leo, na hata milele.

185 Bibi huyu anayeketi kule nyuma kabisa upande huu, karibu na Bi. Wright pale, ana mzigo moyoni mwake. Yeye anaomba kwa ajili ya bintiye. Atafanyiwa upasuaji. Je, unaamini kwa moyo wako wote, kwa ajili yake? Yeye hatauhitaji kama utamfanya kuamini. Mimi siwezi kumponya.

186 Kule nyuma kabisa kwenye chumba cha watoto, namwona Roho Mtakatifu wa Mungu, ama Malaika, Nuru inayotulia katika chumba cha watoto. Imetulia juu ya kijana mwanamke, naye ana shida ya rohoni ambayo inamsumbua. Inaonekana kama yanipasa kumjua huyo mwanamke, kwa vyo vyote. Mwanamke kijana, ana shida ya kike pia. Naam. Jina Lake ni Bi. West, kutoka Alabama, Bi. David West. Amini, na Mungu atakujalia hayo.

187 "Kutakuweko Nuru, na siku ile anapofunuliwa Mwana wa Adamu." Kama huyo si Yesu Kristo yeye yule jana, leo, na hata milele, sijui cho chote kuhusu Hilo. Je, mnaamini Hilo? Mambo yote yanawezekana kwao waaminio.

188 Kule nje kwenye vipaza sauti nchini mwote sasa, na katika Maskani haya, wangapi wenu watainua mikono yenu na kusema, "Mimi ni mwamini"? Sasa, ninyi nje kule nchini, kila mmoja aliyeinua mkono wake hapa; na nje kule mbali sana mahali fulani nchini kote, mlioinua mikono yenu, bila shaka. Basi fungeni macho yenu, wekelea mikono yako juu ya mtu fulani karibu nawe. Shika mkono wake. Uwekelee mbegani mwake. Mimi nimeweka mikono yangu juu ya hizi leso. Tazama yale yametendwa leo! Tazama yaliyotendwa sasa:

Kuutazama uso Wake mbarikiwa
Unaong'ara kwa upendo wa Kiungu;
Washiriki wabarikiwa wa neema Yake,
Watang'ara kama vito kwenye taji Yake.

Basi ombeni. Na tuombe, kila mahali.

189 Mungu mpendwa, wakati umewadia. Je, hii ina maana gani? Mungu akitimiza Neno Lake! Je, kuna mvuto gani Bwana? Ni

Mungu akitimiza Neno Lake. Ni nini kote nchini, kupitia kwa simu, ambapo mamia ya watu wamewekeleana mikono wao kwa wao kote taifani, pwani kwa pwani, kutoka Kaskazini hata Kusini, Mashariki hata Magharibi? Hapa wameketi watu kutoka nchi za ng'ambo, nchi nyingi, Mexico, Canada, nasi tumewekeleana mikono. Mungu anatimiza Neno Lake!

190 Inawezekanaje kwamba mtu anaweza kusimama hapa kwa Roho Mtakatifu na kumtambua mtu kama alivyomfanyia Simoni Petro, "Jina lako ni Simoni, wewe ni mwana wa Yona"?

"Nenda kamwite mumeo mje hapa."

"Sina mume."

"Hakika, una watano."

191 Yeye akasema, "Najua ya kwamba Masihi yuaja kufanya haya, bali Wewe ni nani?"

Akasema, "Mimi Ndiye."

192 Nawe ni yeye yule jana, leo, na hata milele. Nawe umeahidi, "Kazi nizifanyazo mimi, nanyi mtazifanya pia. Naam, na kubwa kuliko hizo mtazifanya, kwa kuwa mimi naenda kwa Baba. Na, tazama, siku za mwisho nitawapelekeeni Eliya, nabii, naye atabadilisha mawazo ya watu, ageuze mioyo ya watoto ielekee Mafundisho ya mitume ya Biblia. Na kutakuweko Nuru yapata wakati wa jioni."

193 Tuko hapa, Mungu mkuu wa Mbinguni! Wakati umewadia! Mikono iko juu ya watu.

194 Shetani, umeshindwa. Wewe u muongo. Na, kama mtumishi wa Mungu, na kama watumishi, tunakuamuru ya kwamba katika Jina la Yesu Kristo, ya kwamba utii Neno la Mungu na utoke ndani ya watu, kwa maana imeandikwa, "Katika Jina Langu watatoa pepo."

195 Na watu wote wawekwe huru. Tujalie, Mungu mpendwa. Wewe ndiye Mungu wa Mbinguni uliyeshinda, siku hiyo kwa mvuto juu ya Mlima Kalvari, magonjwa yote na maradhi na kazi zote za Ibilisi. Wewe ni Mungu! Na watu wameponywa kwa mapigo Yako. Wao ni huru. Katika Jina la Yesu Kristo. Amina.

196 Mungu, kila leso iliyo hapa, wakati Roho wa Mungu yuko, wakati upako wa Yesu Kristo umo juu ya watu, na ishara zile kuu alizoahidi tayari zinatimizwa, na dunia inatetemeka, matetemeko ya nchi yanatokea, zile ishara kuu alizosema, na Maandiko yanatimizwa, na Nuru ya jioni inamulika. Nalalia hizi leso kwa mwili wangu nikiwakilisha mwili huu wote wa waamini kutoka Mashariki, Magharibi, Kaskazini, na Kusini, na kumwambia Ibilisi, "Katika Jina la Yesu Kristo, mwache kila mgonjwa atakayewekelewa hizi," kwa ajili ya heshima na utukufu wa Neno la Mungu. Katika Jina la Neno la Mungu, Yesu Kristo wa Nazarethi. Amina.

197 Sasa, kwa utulivu, busara, kiasi, na kwa uangalifu, kama waamini, je, sasa mnaamini na kukubali uponyaji wenu kutoka kwa Mungu Mwenyezi, katika Jina la Yesu Kristo? Kama ndivyo, inueni mikono yenu. Nyote mlio huko nchini, inueni mikono yenu huko. Kila mtu humu ndani, umbali niwezao kuona, wameinua mikono yao; ndani, nje, kuegemea dirishani, ndani, kule kwenye vyumba vya watoto, kila mahali, watu wameinua mikono yao. Wanakubali. Shetani ameshindwa! Mapigo ya Yesu Kristo yaliwaponya, na Uwepo wa Yesu Kristo unashuhudia jambo kwamba Yeye yu hai leo, awezaye daima kutimiza kila ahadi Yeye aliyoahidi. Amina! Namwamini. Nanyi je?

198 Sasa hebu tusimame. Kwa Jina la Yesu Kristo, tunapokubali yale yaliyotendwa ama yote yaliyosemwa, tunampenda kwa mioyo yetu yote. Tunamthamini kwa yale yote yaliyo ndani yetu. Na sasa mnapoenda manyumbani mwenu mbali mbali usiku wa leo, Mungu awe nanyi. Mungu na awape Roho Mtakatifu iwapo hamna Roho Mtakatifu.

199 Kila mwanamume, mwanamke, kijana, ama msichana, hapa, ambaye hajabatizwa katika Jina la Yesu Kristo, mna nguo, bwana. Usiahirishe mpaka kesho mambo yanayoweza kufanywa leo. Kesho huenda ikawa imechelewa sana. "Yatosha kwa siku maovu yake." Kuna wahudumu wamesimama wanangojea, nguo zinagojea. Hamna kutoa udhuru. Unangoja? Kama unafanya hivyo, nawe unaamini . . . Haidhuru umebatizwa namna gani, kunyunyiziwa maji, kumwagiwa, vyo vyote vile, ni kosa. Nuru imekuja. Njoo, amini, na kubatizwa.

200 Kila mtu asiye na Roho Mtakatifu, na ampokee Roho Mtakatifu, kila mmoja wenu, katika uweza wote wa Kiungu na upendo aliokuahidia, kukufanya kiumbe kipya katika Yeye. Mungu awabariki.

201 Na sasa, hadi Jumapili ijayo asubuhi saa tatu na nusu, hebu na tuimbe wimbo huu mdogo ambao tuliozoea kuimba miaka mingi iliyopita:

> Msisahau maombi ya kijamaa,
> Yesu anataka kukutana nanyi hapo;
> Atawaondolea mashaka yenu yote,
> Msisahau maombi ya kijamaa.

Hebu na tuimbe pamoja sasa:

> Msisahau maombi ya kijamaa,
> Yesu anataka kukutana nanyi hapo;
> Atawaondolea mashaka yenu yote,
> Msisahau maombi ya kijamaa.

202 Sasa, tunapouimba tena, muamkue msafari aliye karibu nawe, unaona, tunapouimba:

Msisahau maombi ya kijamaa,
Lo, Yesu anataka kukutana nanyi hapo;
Atawaondolea mashaka yenu yote,
Lo, msisahau maombi ya kijamaa.

203 Je, ninyi hamumpendi? Mimi nampenda. Nampenda kwa sababu alinipenda kwanza na kununua wakovu wangu (huo ndio mvuto ule) juu ya Mlima Kalvari. Mvuto ule ule juu ya Mlima Sunset, Mlima Nebo, Mlima Sinai, matukio ya juu ya milima ile yote mbalimbali, saba. Naam, hebu na tuuimbe sasa:

Ninampenda, ninampenda
Kwa kunipenda kwanza
Kaninunulia wokuvu
Kalvari.

204 Wote wampendao, waseme “Amina.” Naam, waza tu yale amekutendea. Waza, ya kwamba ungalikuwa kule kwenye pombe usiku wa leo. Huenda ikawa labda ungekuwa kaburini jinsi ningalikuwa, nje ya neema za Mungu. Je, alikufanyia nini? Jamani, tungejizuiaje kumpenda? Haidhuru mtu ye yote asemayo, Yeye ni wa kwanza!

205 Hebu na tufunge macho yetu na kuinamisha vichwa vyetu tunapomwimbia sasa. Yeye hupenda nyimbo, kuimba nyimbo. Hebu na tukamwimbie sasa.

Ninampenda, ninampenda
Kwa kunipenda kwanza
Kaninunulia wokovu
Kalvari.

206 Huku vichwa vyetu na mioyo yetu imeinamishwa katika Uwepo Wake, tukifurahia yale macho yetu yameona, yale masikio yetu yamesikia, yale yameandikwa katika Neno la Mungu, yale ahadi Yake imekuwa kwetu leo. Mungu awabariki.

207 Tuna m—mgeni usiku wa leo, ndugu fulani, Ned Iverson, aliyekuwa muhudumu Mpresbateria. Baba yake, ndugu zake ni wahudumu Wapresbateria. Yeye, nasikia, alibatizwa tena leo katika Jina la Yesu Kristo. Yeye ni muhudumu, mzuri sana kwa kazi hiyo. Na sasa nitamuomba, kwa maana naamini ya kwamba yeye ni mtumishi wa Mungu, kuomba baraka za Mungu juu ya kusanyiko hili mnapoenda nyumbani.

208 Ndugu Iverson, njoo mbele, tunapoinamisha vichwa vyetu kwa maombi. Mungu akubariki, ndugu yangu.

*Nini Kinachovutia Kule Mlimani?* SWA65-0725E
(What Is The Attraction On The Mountain?)

Ujumbe huu uliohubiriwa na Ndugu William Marrion Branham, uliotolewa hapo awali katika Kiingereza mnamo Jumapili jioni, Julai 25, 1965, katika Maskani ya Branham huko Jeffersonville, Indiana, Marekani, umetolewa kwenye kanda ya sumaku iliyorekodiwa na kuchapishwa bila kufupishwa katika Kiingereza. Tafsiri hii ya Kiswahili ilichapishwa na kusambazwa na Voice Of God Recordings.

SWAHILI

©2004 VGR, ALL RIGHTS RESERVED

Voice Of God Recordings
P.O. Box 950, Jeffersonville, Indiana 47131 U.S.A.
www.branham.org

Ilani ya haki ya kunakili

Haki zote zimehifadhiwa. Kitabu hiki kinaweza kuchapishwa kwa matbaa ya nyumbani kwa matumizi ya kibinafsi ama kusambaza, bila malipo, kama chombo cha kuitangazia Injili ya Yesu Kristo. Kitabu hiki hakiwezi kikauzwa, kunakiliwa kwa wingi, kuwekwa kwenye mtandao, kuhifadhiwa kikatolewe tena, kufasiriwa katika lugha zingine ama kutumiwa kuomba fedha bila idhini halisi iliyoandikwa moja kwa moja kutoka Voice Of God Recordings®.

Kwa habari zaidi ama kwa vifaa zaidi, tafadhali wasiliana na:

VOICE OF GOD RECORDINGS
P.O. BOX 950, JEFFERSONVILLE, INDIANA 47131 U.S.A.
www.branham.org